BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KIDATO CHA SITA, 2016

## 121 KISWAHILI

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KIDATO CHA SITA, 2016

# 121 KISWAHILI

*Kimechapishwa na*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2016**

Haki zote zimehifadhiwa.

# YALIYOMO

DIBAJI ........ iv
1.0 UTANGULIZI ........ 1
2.0 SEHEMU YA I: KISWAHILI KARATASI YA KWANZA ........ 2
2.1 TATHMINI KWA KILA SWALI ........ 2
2.2 SEHEMU A: UFAHAMU ........ 2
2.2.1 Swali la 1: Ufahamu ........ 2
2.2.2 Swali 2: Ufupisho ........ 6
2.2.3 SEHEMU B: MATUMIZI YA SARUFI NA UTUMIZI WA LUGHA 9
2.2.4 Swali la 3: Matumizi ya Sarufi ........ 9
2.2.5 Swali la 4: Matumizi ya Sarufi ........ 13
2.2.6 Swali la 5: Matumizi ya Sarufi ........ 19
2.2.7 Swali la 6: Utumizi wa Lugha ........ 23
2.3 SEHEMU C: UTUNGAJI ........ 28
2.3.1 Swali la 7: Uandishi wa Insha ........ 28
2.4 SEHEMU D: MAENDELEO YA KISWAHILI ........ 34
2.4.1 Swali la 8: Usanifishaji ........ 34
2.4.2 Swali la 9: Kukua na Kuenea kwa Kiswahili ........ 41
2.5 SEHEMU E: TAFSIRI ........ 45
2.5.1 Swali la 10: Nadharia ya Tafsiri ........ 45
3.0 SEHEMU YA II: MTIHANI WA KISWAHILI KARATASI YA PILI ..... 50
3.1 TATHMINI KWA KILA SWALI ........ 50
3.2 SEHEMU A: FASIHI KWA UJUMLA ........ 50
3.2.1 Swali la 1: Fasihi kwa Ujumla ........ 50
3.2.2 Swali la 2: Fasihi kwa Ujumla. ........ 54
3.3 SEHEMU B: USHAIRI ........ 59
3.3.1 Swali la 3: Uhakiki wa Ushairi ........ 59
3.3.2 Swali la 4: Uhakiki wa Ushairi ........ 65
3.4 SEHEMU C: RIWAYA ........ 72
3.4.1 Swali la 5: Uhakiki wa Riwaya ........ 72
3.4.2 Swali la 6: Uhakiki wa Riwaya ........ 77
3.5 SEHEMU D: TAMTHILIYA ........ 84
3.5.1 Swali la 7: Uhakiki wa Tamthiliya ........ 84
3.5.2 Swali la 8: Uhakiki wa Tamthiliya ........ 92
3.6 SEHEMU E: USANIFU WA MAANDISHI. ........ 98
3.6.1 Swali la 9: Usanifu wa Maandishi ........ 98
3.6.2 Swali la 10: Usanifu wa Maandishi ........ 104
4.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA KUFAULU CHA WATAHINIWA KWA MADA ........ 112
5.0 HITIMISHO ........ 112
6.0 MAPENDEKEZO ........ 113
Kiambatisho A ........ 115
Kiambatisho B ........ 116

# DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kutoa kitabu hiki kinachohusiana na Taarifa ya Uchambuzi wa Majibu ya Watahiniwa katika Mtihani wa Kuhitimu Kidato cha Sita kwa somo la Kiswahili. Taarifa hii imeandaliwa ili kutoa mrejesho wa kufaulu katika mitihani kwa wanafunzi, walimu, wazazi, waandaaji wa sera na wadau wa elimu kwa ujumla.

Taarifa hii ni tathmini ya mwisho inayolenga kuonesha mafanikio ya mfumo wa elimu kwa ujumla hususani katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Kimsingi uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mtihani huu unalenga kuonesha dhahiri maarifa ambayo mfumo wa elimu uliweza au ulishindwa kuwapa watahiniwa walipokuwa katika elimu ya Sekondari.

Uchambuzi uliowasilishwa katika taarifa hii una lengo la kuchangia katika kuelewa zaidi sababu za watahiniwa kufanya vibaya au vizuri au kwa kiwango cha wastani katika mtihani huo. Taarifa hii inaonesha baadhi ya sababu zilizofanya watahiniwa wengi kufanya vizuri. Aidha, sababu zilizofanya watahiniwa wachache kutopata alama za juu katika majibu yao zimefafanuliwa pia. Sababu hizo ni kama vile kutoelewa matakwa ya swali, uwezo mdogo wa watahiniwa wa kujieleza kwa lugha fasaha na udhaifu katika kuelewa dhana zinazohusiana na somo la Kiswahili. Mrejesho huu utawawezesha viongozi wa elimu, viongozi wa shule, walimu na wanafunzi kupata mbinu muafaka katika kuboresha kufaulu kwa watahiniwa katika mitihani ijayo inayotolewa/inayoendeshwa na Baraza la Mitihani la Tanzania.

Baraza la Mitihani la Tanzania litapenda kupokea maoni na mapendekezo kutoka kwa walimu, wanafunzi na umma kwa ujumla, ambayo yatatumika katika kuboresha taarifa za watahini zitakazofuata.

Mwisho Baraza linapenda kuwashukuru Maafisa Mitihani, walimu wa somo na wengine wote waliohusika katika kutayarisha taarifa hii. Tunapenda vilevile kutoa shukrani zetu za pekee kwa wafanyakazi wa Idara ya Utafiti Tathmini na Huduma za Kompyuta walioshiriki katika uchambuzi wa data zilizotumika katika ripoti hii.

Dr. Charles Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Mtihani wa somo la Kiswahili kwa watahiniwa wa Kidato cha Sita ulifanyika Mei 2016 na ulizingatia muhtasari wa somo la Kiswahili kwa Kidato cha V na cha VI.

Mtihani wa **121/1 Kiswahili** uligawanywa katika sehemu **A, B, C, D** na **E** kwa kuzingatia mada za *Ufahamu*, *Utumizi wa Lugha*, *Matumizi ya Sarufi*, *Utungaji*, *Maendeleo ya Kiswahili* na *Tafsiri na Ukalimani*, ambapo kila sehemu ilikuwa na alama ishirini (20). Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali saba (7) kati ya maswali kumi (10): Sehemu A na B maswali mawili (2) kwa kila sehemu; na sehemu C, D na E, swali moja kwa kila sehemu.

Mtihani wa **121/2 Kiswahili** uligawanywa katika sehemu **A**, **B**, **C**, **D** na **E** kwa kuzingatia mada za *Fasihi kwa Ujumla*, *Ushairi*, *Riwaya*, *Tamthiliya na Usanifu wa Maandishi* ambapo kila sehemu ilikuwa na alama 20 na kila mtahiniwa alitakiwa kujibu swali moja tu kwa kila sehemu, hivyo kutakiwa kujibu jumla ya maswali matano (5).

Kufaulu kwa watahiniwa katika mtihani wa 121 Kiswahili kwa mwaka 2016 kulikuwa kwa kiwango kizuri ambapo asilimia **99.94** ya watahiniwa wote waliofanya mtihani walipata wastani wa alama 35 na zaidi. Kufaulu huku kumejikita katika viwango vitatu vya kufaulu, ambavyo ni ‘‘vizuri’’, ‘‘wastani’’ na ‘‘hafifu.’’ Kufaulu kwa kiwango kizuri kunaanzia alama 60 hadi 100; kiwango cha wastani alama 35 hadi 59; na kufaulu kwa kiwango hafifu ni alama 0 hadi 34. Aidha, chati za viwango vya kufaulu zimeambatishwa ili kufafanua kufaulu kwa watahiniwa ambapo rangi ya kijani inawakilisha kufaulu kwa kiwango kizuri, rangi ya njano inawakilisha kufaulu kwa kiwango cha wastani na kufaulu kwa kiwango hafifu kunawakilishwa na rangi nyekundu.

Taarifa hii inachambua maswali yaliyojibiwa vizuri, wastani na hafifu ili kukuza kiwango cha ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Uchambuzi huu unalenga kuonesha hali halisi jinsi watahiniwa walivyojibu maswali katika Mtihani wa karatasi ya kwanza 121/1 na ya pili 121/2 ya somo hili la Kiswahili. Sampuli za majibu yao zimeambatanishwa ili kuonesha kilichotarajiwa kufanywa na kilichofanywa na watahiniwa. Aidha, taarifa hii inaonesha pia sababu zilizowafanya watahiniwa wachache kutopata alama za juu katika majibu ya maswali kwa baadhi ya mada. Hivyo, uchambuzi huu umeweka mpango mkakati wa kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa mada hizo ili kuboresha kufaulu kwa watahiniwa katika mitihani yote inayoendeshwa na Baraza la Mitihani la Tanzania.

## 2.0 SEHEMU YA I: KISWAHILI KARATASI YA KWANZA

### 2.1 TATHMINI KWA KILA SWALI


### 2.2 SEHEMU A: UFAHAMU

#### 2.2.1 Swali la 1: Ufahamu

Swali hili lilihusu mada ya *Ufahamu* na lililenga kupima ufahamu. Swali lilimtaka mtahiniwa kusoma kifungu cha habari na kisha kujibu maswali yanayofuata. Maswali hayo yaligawanyika katika vipengele (a) hadi (f) na vilikuwa na jumla ya alama 12.

Kipengele (a) kilimtaka mtahiniwa kuandika kichwa cha habari aliyoisoma kisichozidi maneno matano. Kipengele (b) kilimtaka mtahiniwa kutoa maana za maneno kama yalivyotumika katika habari aliyosoma. Kipengele (c) kilimtaka mtahiniwa ataje faida nne zitokanazo na kuwapo kwa katiba katika Taifa. Kipengele (d) kilimtaka mtahiniwa kutoa maelezo kuhusu msemo alioutumia mwandishi usemao, “Taifa bila Katiba ni sawa na behewa la gari moshi bila ya injini”. Kipengele (e) kilimtaka mtahiniwa kutumia sentensi mbili kuelezea mtazamo wa mwandishi kuhusu jamii iliyostaarabika na kipengele (f) kilimtaka mtahiniwa atoe wazo kuu la mwandishi katika aya ya mwisho.

Swali lilikuwa la lazima na lilijibiwa na asilimia 99.5 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili na kufaulu kwao kiasilimia kumefafanuliwa vizuri katika Chati Na.1 kwa kuonesha kufaulu kwa kiwango hafifu, kufaulu kwa kiwango cha wastani na kufaulu kwa kiwango kizuri.




**Chati Na. 1**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Asilimia 95.2 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata alama 4.5 hadi 12. Miongoni mwao, asilimia 73.8 walipata alama za juu za swali yaani alama 7.5 hadi 12 kutokana na kumudu kujibu vipengele vingi vya swali hili kwa usahihi. Aidha, baadhi ya watahiniwa hao waliweza kuandika kichwa cha habari kama kilivyotakiwa, kutoa maana za maneno kama yalivyotumika katika habari, kutaja faida nne za kuwepo kwa katiba katika Taifa, kutafsiri msemo ‘‘*Taifa bila katiba ni sawa na behewa la gari moshi bila injini*’’, na kuelezea mtazamo wa mwandishi kuhusu jamii iliyostaarabika. Aidha, watahiniwa wengine walitoa majibu ambayo hayakujitosheleza kwa vipengele vyote na hivyo kupata alama pungufu kidogo. Kielelezo 1.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu vipengele (a), (b), (c), (e) na (f) kwa usahihi lakini katika kipengele (d) alitoa jibu lisilohusisha ‘injini’ na ‘gari moshi’ katika kuelezea umuhimu wa katiba kwa taifa kama ilivyotakiwa.

**Kielelezo 1.1**

1 a) UMUHIMU WA KATIBA KATIKA TAIFA.

b i) Uzandiki - Ni kitendo cha watu wanafiki na kutoelewana kwa sababu ya jambo fulani

chombo maalumu ambacho

ii) Katiba - Ni kanuni na taratibu ambazo huongoza jamii kufikia upeo wake kimaendeleo kuanzia ngazi ya chini kabisa ambayo ni familia mpaka ngazi ya juu kabisa ambayo ni Taifa.

iii) Kiimla - Ni nchi zenye utawala wa mabavu au kidikteta ambapo katiba hutayarishwa na watawala kwa maslahi yao wenyewe.

iv) Buruji - Katiba hutumiwa kama njia au mlango wa kujipatia maslahi kwa watawala.

v) Watwana - Wananchi kuwa watumwa katika nchi yao wenyewe.

vi) Muhali - Ni jambo linaloleta mashaka au kushangaza mtu aliyeijua katiba kutoa ~~maa~~ maoni kuhusu katiba.

c Faida nne zinazotokana na kuwepo kwa katiba katika taifa lolote.

i) Katiba huiongoza jamii kufikia upeo wa kimaendeleo katika Taifa.

ii) Katiba huelekeza wajibu wa kila mwanajamii kwa taifa lake.

iii) Katiba hutoa utaratibu wa mchakato wa uongozi wa kisiasa na kijamii na uhuru wa mtu binafsi.

iv Katiba huelekeza haki anazostahili raia katika taifa lake.

1 d/ Mwandishi anaposema "Taifa bila katiba ni sawa na behewa la gari moshi bila injini anamaanisha kuwa nchi bila katiba haiwezi kupata maendeleo kwa sababu ili nchi iweze kufikia upeo wake kimaendeleo kuanzia ngazi ya chini kabisa hadi ya juu kabisa ni lazima kuwepo Katiba.

e/ Jamii iliyostaarabika wananchi wake hutambua, kuheshimu na kuthamini uwepo wa katiba. Watawala wasiwe kama wateule wa maulana na kutotumia mabavu bali waheshimu katiba.

f/ Wazo kuu la mwandishi katika aya ya mwisho ni kuwa wananchi wanahitaji kuelimishwa ili kuweza kuwa na uelewa wa kutosha juu ya suala la katiba ili kuweza kutambua, kuheshimu na kuthamini uwepo wa katiba kama njia muafaka ya kuleta maendeleo kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni.


Kielelezo 1.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kujibu vipengele (a), (b), (c), (e) na (f) kwa usahihi isipokuwa kipengele (d) alishindwa kuhusisha dhana ya injini katika gari moshi na umuhimu wa katiba kwa taifa kiuhalisia.

Asilimia 21.4 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani yaani alama 4.5 hadi 7 kutokana na kujibu kwa usahihi baadhi ya vipengele na vipengele vingine vilikuwa na majibu ambayo hayakujitosheleza. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alijibu vipengele (a), (c) na (d) kwa usahihi lakini kipengele (b) kilichomtaka kueleza maana za maneno alitoa maana iliyo kinyume na maneno hayo kama vile neno 'Muhali' – *rahisi au vyepesi*, ambapo jibu sahihi lilitakiwa liwe *jambo gumu au kutowezekana/adimu.*

Aidha, watahiniwa wachache (4.8%) walijibu vibaya vipengele vingi vya swali hili na kupata alama 0 hadi 4. Baadhi ya watahiniwa katika kundi hili walikuwa na uelewa kuhusu mada ya ufahamu lakini walikosa umakini katika majibu yao. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika kipengele (a) aliandika kichwa cha habari kwa herufi ndogo badala ya herufi kubwa, na katika kipengele (b) (i), (iii) na (iv) alitoa maana ambazo sio sahihi kulingana na kifungu cha habari ijapokuwa katika kipengele (ii), (v) na (vi) aliweza kutoa maana sahihi. Katika kipengele (c), (d),

(e) na (f), mtahiniwa huyo alitoa majibu ambayo hayakujitosheleza. Kielelezo 1.2 kinafafanua majibu ya mtahiniwa wa aina hiyo.

Kielelezo 1.2


1a Katiba.
b i - Mzandiki = Uongo.
ii - Katiba. = Chombo maalumu cha kuweka kanuni na taratibu.
iii Kiini mla = utaratibu uliokuwa hauzingatii haki
iv. buruji = Njia ya maendeleo.
v. Watwana = Watumwa.
vi. muhali. = Vigumu.
c - Kuimarika kwa umoja.
- Kuimarika kwa mashirikiano
- Kupatikana kwa maendeleo.
- Kuimarika kwa uchumi na kupata kiongozi bora.
d. Anamaanisha kuwa Taifa bila katiba maendeleo yatakuwa ni duni kupatikana kwani gari moshi bila injini haiwezi kwenda.
e Mkazo kuu la mwandishi katika ubeti wa mwisho ni muhimu


Kielelezo 1.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetoa majibu yasiyojitosheleza katika vipengele (a) hadi (d) na kutojibu kabisa kipengele (f).

### 2.2.2 Swali 2: Ufupisho

Swali lilihusu mada ya *Ufupisho* na lililenga kupima matumizi. Swali lilimtaka mtahiniwa kufupisha habari aliyoisoma kwenye swali la kwanza kwa maneno mia moja na ishirini (120) na lilikuwa na jumla ya alama 8.

Swali lilijibiwa na asilimia 96.4 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani kwa kuwa lilikuwa ni la lazima. Watahiniwa wengi, (96.2%) waliojibu swali hili walipata alama 3 hadi 8. Miongoni mwao, asilimia 62 ya watahiniwa hao walipata alama 5 hadi 8 kwa kuwa waliweza kuzingatia kanuni na taratibu za kufupisha habari kwa viwango tofauti. Baadhi ya watahiniwa katika kundi hili walijibu swali hili vizuri zaidi kwa kuwa waliweza kutumia maneno yao wenyewe bila kupotosha kiini cha habari ya awali, kuzingatia mtiririko mzuri wa mawazo wenye mantiki, matumizi ya lugha sanifu na idadi ya maneno iliyoendana na matakwa ya swali. Watahiniwa wengine walijibu vizuri lakini majibu yao yalikuwa na upungufu kwa baadhi ya vigezo muhimu katika ufupisho wa habari. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifupisha habari bila kuzingatia mtiririko wa mawazo wenye mantiki kwa kila aya na hivyo kutopata alama zote. Kielelezo 2.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyefupisha habari kwa kuzingatia vigezo muhimu lakini akashindwa kuzingatia kanuni muhimu za uandishi.

**Kielelezo 2.1**


2. Katika Taifa lolote duniani kuwepo chombo cha uongozi wa viongozi na raia. Chombo hicho huitwa Katiba. Katiba huchukuwa kanuni za nchi na huonesha majukumu mbali mbali.

Katiba huonesha wajibu wa raia kwa taifa na hata viongozi. Pia hutaja haki na mabadilishano ya uongozi. Katiba hulinda majukumu ya kiongozi. Bali pia katiba hulinda utamaduni wa Taifa.

Katiba hupatikana kutokana na michango ya maoni ya wananchi wenyewe.

Hivyo wananchi hawana budi kufahamu maana ya katiba na kushiriki kutoa maoni yao na kushinikizana wao kwa wao juu ya umuhimu wa katiba. Pia watawala wasijivishe jukumu la kupitisha katiba bila ya maoni ya raia kwani ni uvunjifu wa demokrasia.


Kielelezo 2.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri ijapokuwa hakuzingatia kanuni za uandishi wa herufi kubwa.

Aidha, asilimia 34.2 ya watahiniwa waliofanya swali hili walikuwa na kiwango cha kufaulu cha wastani kutokana na kushindwa kuzingatia baadhi ya vigezo vya ufupisho kwa ukamilifu wake. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifupisha habari kwa kuyapanga mawazo na kutumia maneno yake mwenyewe bila kuzingatia idadi ya maneno na matumizi ya lugha sanifu na hivyo kupata alama za wastani.

Watahiniwa wachache, (3.8%) pekee ndio ambao hawakujibu swali hili vizuri na walipata alama 0 hadi 2.5. Asilimia 0.7 ya watahiniwa katika kundi hili walipata alama 0 kutokana na kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu kifungu cha habari walichosoma na hivyo kushindwa kufupisha habari kwa kuzingatia alama za uandishi, kutumia maneno yao wenyewe na

kuwa na mtiririko wa mawazo wenye mantiki na pia hawakuzingatia matumizi ya lugha sanifu. Kielelezo 2.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyefupisha habari bila kuzingatia idadi ya maneno, mtiririko wa mawazo wenye mantiki na kurudia baadhi ya maneno yaliyotumika katika habari.

**Kielelezo 2.2**


2 Ustaarabu ni jambo ambapo hupendwa na kila mtu. Kila penye ustaarabu kuna kanuni zimewe kwa. Watu huto maamuzi bila hamaki na uzandiki; huo ngoza jamii kufika katika maendeleo. Kanuni hizo huwe kwa na taifa ambazo huitwa katiba.

Katika nchi zenye demokrasia katiba huundwa kwa maoni ya wananchi; Sehemu ya utawala wa kinyume na hilo katiba ni viongozi ambao hu fuata matakwa ~~yote ya~~ yao wenyewe; hivyo wananchi huwa ni watwana.

Wananchi ni vizuri kuzidewa maana ya katiba.

Kielelezo 2.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeandika ufupisho kwa kunakili maneno kama yalivyo katika habari aliyopewa bila ya kuzingatia mtiririko wa mawazo wenye mantiki.


### 2.2.3 SEHEMU B: MATUMIZI YA SARUFI NA UTUMIZI WA LUGHA

### 2.2.4 Swali la 3: Matumizi ya Sarufi

Swali lilihusu mada ya *Matumizi ya Sarufi* na lilimtaka mtahiniwa kufafanua kuhusu dhana ya ‘Uainishaji wa Ngeli za Nomino’ kwa kigezo cha kisintaksia, kisha kwa kutumia mifano kutoa hoja nne zinazoonesha umuhimu wa uainishaji huo katika lugha ya Kiswahili. Swali hili lililenga kupima matumizi na lilikuwa na jumla ya alama 10.

Swali lilijibiwa na watahiniwa wachache zaidi katika sehemu hii ambapo asilimia 23.4 pekee ndio waliojibu kati ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Asilimia 72.8 ya watahiniwa hao waliojibu walipata alama 3.5 hadi 10. Miongoni mwao, asilimia 38 walijibu vizuri na kupata alama 6 hadi 10 kutokana na kuwa na maarifa na uelewa kuhusu mada ya *Ngeli za Nomino* kwa viwango tofauti. Baadhi ya watahiniwa waliojibu vizuri zaidi waliweza kufafanua dhana ya 'Uainishaji wa Ngeli za Nomino' kwa kigezo cha kisintaksia, kisha kuonesha umuhimu wa uanishaji huo katika lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kuonesha umuhimu wa uanishaji ngeli kisintaksia kama; *uhusiano uliopo baina ya Kiswahili na lugha za Kibantu, umoja na wingi katika sentensi za Kiswahili, kuonesha upatanisho wa kisarufi, na kupanga majina katika makundi yanayofanana.* Kielelezo 3.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyefanya vizuri kwa kufuata matakwa ya swali.

**Kielelezo 3.1**


2. Ngeli za majina kwa kigezo cha kisintaksia, Ni ugawaji wa ngeli za nomino kulingana na maana halisi ya nomino husika. Uanishaji huu una umuhimu katika lugha ya Kiswahili kama inavyoonekana hapo chini:

∴ Kuonesha uhusiano uliopo baina ya Kiswahili na lugha za Kibantu. Mfano, katika ngeli ya kwanza ya A-WA


Kiswahili
Mtoto Anakula
Watoto Wanakula

Kihaya
Omwana Nalya
Abhana Mbalya

Kuonesha umoja na wingi katika sentensi za Kiswahili. Mfano katika ngeli ya KI-VI

Umoja Wingi
Kiti Viti
Kijiko Vijiko
Kidole Vidole

Kuonesha upatanisho wa kisarufi katika sente



3. Ngeli za Majina kwa kigezo cha kisintaksia, Ni ugawaji wa ngeli za nomino kulingana na maana halisi ya nomino husika. Uainishaji huu una umuhimu katika lugha ya Kiswahili kama inavyoonesha hapo chini:

∴ Kuonesha uhusiano uliopo baina ya Kiswahili na lugha za Kibantu. Mfano, katika ngeli ya kwanza ya A-WA

Kiswahili
Mtoto Anakula
Watoto Wanakula

Kihaya
Omwana Nalya
Abhana Mbalya

Kuonesha umoja na wingi katika sentensi za Kiswahili. Mfano katika ngeli ya KI-VI

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Kiti | Viti |
| Kijiko | Vijiko |
| Kidole | Vidole |

Kuonesha upatanisho wa kisarufi katika sente-

3 sentensi za Kiswahili. Mfano katika ngeli ya Li-Ya pamoja na Ji-Ma.

Umoja
Embe limeanguka
Maembe Yameanguka

Kuonesha "O" rejeshi katika sentensi za Kiswahili. Mfano katika ngeli ya Li-Ya

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Lililoiva | Yaliyoiva |
| -Lo- | -Yo- |

I-Zi


| | |
|---|---|
| Ilioibiwa | Zilizoibiwa |
| -O- | -Zo- |

Kielelezo 3.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri kwa kufafanua dhana ya 'Uainishaji wa Ngeli za Nomino' kwa kigezo cha kisintaksia na kutoa hoja nne zinazoonesha umuhimu wake katika lugha ya Kiswahili.

Aidha, watahiniwa wengine (34.8%) walipata alama za wastani yaani alama 3.5 hadi 5.5 kutokana na kukosa maarifa ya kutosha kuhusu umuhimu wa uainishaji ngeli kisintaksia katika lugha ya Kiswahili. Majibu ya watahiniwa hao yalikuwa na upungufu katika kufafanua dhana ya uainishaji wa ngeli za nomino kwa kigezo cha kisintaksia na hivyo kushindwa kupata alama zote za swali.


Watahiniwa wachache (27.2%) walipata alama chini ya wastani yaani alama 0 hadi 3. Watahiniwa hao walishindwa kufafanua kuhusu dhana ya 'Uainishaji wa Ngeli za Nomino' kwa kigezo cha kisintaksia na kuonesha umuhimu wake katika lugha ya Kiswahili kwa viwango tofauti. Baadhi yao hawakuelewa kabisa matakwa ya swali na hivyo kutoa majibu kama vile; ngeli ya -KU- husaidia katika kunominisha, Ngeli ya KI-VI husaidia kuonesha O-rejeshi, ngeli ya I – ZI husaidia kuonesha njeo ya wakati, majibu ambayo hayakuwa sahihi. Kielelezo 3.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.

**Kielelezo 3.2**


3. Uainishaji wa ngeli ni kitendo cha kuziweka ngeli tofauti na katika makundi ili yaweze kuleta maana husika. Mfano, KI-VI, YU-A-WA, U-ZI, n.k ili kuweza kubainisha Nomino husika.

Ngeli ya -KU- ambapo ngeli hii husaidia katika kunominisha nomino husika katika sentensi Mfano: Kucheza kwake kunavutia. Hivyo ngeli hii imesaidia kuonesha mtendo kufanya nini

Ngeli ya KI-VI husaidia kuonesha O-rejeshi ambapo ili kuweza kukamilisha sentensi husika Kiatu kilichopotea kimepatikana na vilevile



3. Viato vilivyopotea vimepatikana na hii kusaidia kuonesha J Orejelshi katika sentensi

Ngeli ya I-ZI hii ngeli husaidia katika kuonesha njia ya wakati uliopita na timilifu hapa Mfano: Nguo imechanika na Nguo zimechanika, na hapa ngeli hii kuonesha bayana wakati


Ngeli ya LI-YA hii ni ngeli ambayo huonesha wakati uliopo na kwa kufanana ambapo Mfano, Embe limeoza na Maembe Yameoza kuonesha tukio linalotendeka kwa wakati huo huo uliopo

Kielelezo 3.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kufafanua dhana ya uainishaji wa ngeli za nomino kwa kigezo cha kisintaksia na kutoa hoja nne ambazo zilikuwa ni kinyume na matakwa ya swali.

### 2.2.5 Swali la 4: Matumizi ya Sarufi

Swali lilitoka katika mada ya *Matumizi ya Sarufi* na lilimtaka mtahiniwa kueleza maana ya vivumishi na viwakilishi kisha kuonesha kufanana na kutofautiana kati ya vivumishi na viwakilishi. Swali lilikuwa na alama 10 na lililenga kupima tathmini.

Swali lilijibiwa na watahiniwa wachache ambao ni asilimia 25.7 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili na kufaulu kwao kiasilimia kumewasilishwa vizuri katika Chati Na.2 kwa kuonesha kufaulu kwa kiwango hafifu, kufaulu kwa kiwango cha wastani na kufaulu kwa kiwango kizuri.




**Chati Na. 2**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Asilimia 52.4 pekee ndio walioweza kupata alama 3.5 hadi 10. Kati yao, watahiniwa wachache (14.6%) walilijibu vizuri na walipata alama 6 hadi 10 kwa kuwa waliweza kueleza maana ya vivumishi na viwakilishi na kutoa hoja za kufanana na kutofautiana kati ya vivumishi na viwakilishi kwa viwango tofauti. Watahiniwa waliojibu vizuri zaidi waliweza kutoa hoja nne za kufanana na kutofautiana kati ya vivumishi na viwakilishi kama vile, Kufanana: *Vyote huonesha umbali/ukaribu wa vitu, huweza kuwa katika mfumo wa kuuliza swali na vyote huwa na umilikishi* na kutofautiana*: Vivumishi hutokea baada ya nomino, havibebi mofimu za nafsi na havioneshi mahali lakini viwakilishi husimama badala ya nomino, hubeba mofimu za nafsi na huonesha mahali*. Watahiniwa wengine katika kundi hili walitoa hoja chache katika kutofautisha na kufananisha vivumishi na viwakilishi. Kielelezo 4.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejitahidi kutoa hoja za kufanana na kutofautiana kati ya vivumishi na viwakilishi.

**Kielelezo 4.1**

04 Vivumishi ni maneno ambayo hutoa
sifa za Nomino na pia sifa za Viwakilishi
lakini Viwakilishi ni Maneno ambayo husi
mama badala ya Nomino. Katika sarufi
Miundo Maneno huwa yanabaguliana na
Kutenana katika sentensi ili Kuleta
Maana kamili iliyokusudiwa.
Zifuatazo ni hoja ambazo huonesha
ufanano kati ya Kivumishi na Kiwakilishi
Vivumishi na Viwakilishi vyote hudo
kera Idadi ya vitu vilivyopo au visivyo
Kuwepo. Idadi inaweza Kuwa ile inayo
julikana au isiyojulikana Kwamfano.
Maneno kama vile Wachache, Wengi, Watoto,
Sita na Chungu nzima Viwakilishi na
Vivumishi huyatumia na Kuonesha ufanano
fulani.
Vivumishi na Viwakilishi huonesha
Mahali pa karibu au pa mbali sana au
Mbali Kiasi Maneno kama vile Kule, pale,
na Mule vyote huyatumia Kwa matumizi
Matumizi mazuri.
Vivumishi na Viwakilishi huonesha
Kumilikisha Kwa jambo au Kitu fulani
ambacho chaweza Kuwa ni Chako au
cha Mwingine Maneno yanayotumika ni
yamoja na Chako, Chake, Changu na
yako vyote vivumishi na viwakilishi hutu
mia na Kuonesha Kwamba Kuna ufanano
Pia Vivumishi na Viwakilishi huwa
Vinaonesha au huuliza jambo fulani kama
limetendeka hau halijatendeka au la

Kushituka au la fulana Kwamfano ~~Wanggi~~ Wangapi?, vyote vivumishi na viwakilishi huutiza jambo fulani na kuonesha ufanano fulani wa jambo hilo katika uwakilishi na uvumishi wake.

Pia kutokana na ufanano wa vivumishi na viwakilishi kuna utofauti mkubwa kati ya viwakilishi na vivumishi kama ifuatavyo;

Kivumishi ni maneno ambayo huto a sifa za Nomino au kiwakilishi chenye we lakini kiwakilishi ni maneno amba yo hutumika kusimama badala ya Nomino, Hivyo huonesho kuna utofauti mkubwa kati ya vivumishi na viwakili shi.

Kivumishi hutangulia Nomino au kiwakilishi katika muundo ya sentensi kwa sababu huwezi kuanza kivumishi halafu uje kiwakilishi, Ukianza kivumishi hicho tena si kivumishi bali ni kiwakili shi cha Nomino kwa mfano

Mzuri anapika huwezi kusema
W T

Mzuri ni kivumishi bali kinawakilisha no mino.

Kivumishi na kiwakilishi hutofau tiana kati aina kwani kivumishi kina aina chache sana lakini kiwakilishi huwa na aina nyingi zaidi ya saba hivyo huonesha utofauti mkubwa kati ya kivumishi na kiwakilishi.

Pia Kivumishi na Kiwakilishi huto-
fautiana katika kuanza kwamba Kivumishi
hakiwezi kuanza mwanzoni mwa sentensi
bali huanza kiwakilishi halafu Kivumishi
Pia Kivumishi chaweza kukosekana kati
ka sentensi bila kuharibu maana ya
sentensi. Kwa mfano:-

Yule anacheza

W

Kivumishi katika sentensi hiyo hakipo bali
kipo Kiwakilishi na Kitenzi.

Hitimisho, Makosa mengi ya Kisaru
fi huwa yanatokea kwa kutofuata sarufi
Miundo yaani ile sarufi ambayo huwa
Maneno yanatenkana na kubagukana
katika sentensi Kwamfano.

Juma anacheza mpira vizuri sana

N T N E

Halafu mwingine anaanza na Kielezi, anafuata
Kitenzi anamalizia Nomino. Sarufi Miundo
katika kutumia maneno huwa tunaanza
na Nomino au Kiwakilishi Kisha tuna
fuata Kivumishi sio Kivumishi halafu
Kiwakilishi.


Kielelezo 4.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyefanya vizuri swali hili ijapokuwa alitoa hoja pungufu katika kutofautisha viwakilishi na vivumishi.

Asilimia 37.8 ya watahiniwa walipata alama za wastani ambazo ni alama 3.5 hadi 5.5. Watahiniwa hao hawakuweza kufafanua kufanana na kutofautiana kati ya vivumishi na viwakilishi kwa ukamilifu. Baadhi yao walitoa mfanano tu bila ya kutoa tofauti na wengine walitoa tofauti tu bila ya kueleza mfanano.

Asilimia 47.6 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 0 hadi 3 kwa kuwa hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dhana ya vivumishi na viwakilishi. Baadhi ya watahiniwa hao walishindwa kuonesha tofauti na mfanano kati ya vivumishi na viwakilishi na wengine waliweza tu kutoa maana ya dhana hizo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alishindwa kufananisha na

kutofautisha dhana ya vivumishi na viwakilishi kwa kufafanua dhima za viambishi huku akitoa mifano ya maneno yasiyohusiana na dhana hiyo kama vile; *kutia chumvi katika sentensi*; *kuongeza uzuri wa sentensi* na *hali ya kusisitiza jambo*. Kielelezo 4.2 ni mfano wa jibu la mtahiniwa wa aina hiyo.

**Kielelezo 4.2**


4 Vivumishi ni viambishi vinavyo vumisha kitu katika sentensi na viwakilishi ni viambishi vinavyo wakilisha kitu katika sentensi zifuatazo ni hoja nne kuonesha kufanana na hoja nne kuonesha kutofautisha kati ya vivumishi na viwakilishi kwa kuanza na vivumishi kamalifuatavyo

Kuvumisha maneno katika sentensi mfano Juma anaongea mzuri sana ✓

Kuonesha hali ya kusisitiza jambo au kutilia mkazo wakiti Mfano unatakiwa kufika bila kukosa

Kutia chumvi katika sentensi Mfano Juma alikimbia haraka kama farasi ✓

Kuongeza uzuri wa sentensi Mfano Maji ni matamu kama sega la Asali. ✓

Kwa kuhitimisha na viwakilishi

Kuwakilisha neno fulani katika sentenzi

Mfano Mwalimu Juma K

Kuweka kitu kingine badala ya kitu halisi katika sentensi Mfano Asha ni mzuri kama malaika

4 Kutoa uwakilishi katika sentensi

Kufanya sentensi iwe bora na nzuri katika uboraji wake

Kwa kuhitimisha Maana ya vivumishi na viwakilishi vimeweza kufafanuliwa katika hoja nne hapo juu.

Kielelezo 4.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kufananisha na kutofautisha viwakilishi na vivumishi kwa kufafanua dhima za viambishi kinyume na matakwa ya swali.

### 2.2.6 Swali la 5: Matumizi ya Sarufi

Swali lilihusu mada ya *Matumizi ya Sarufi* na lililenga kupima uchambuzi. Swali lilimtaka mtahiniwa kutaja na kufafanua kwa mifano vipashio vitano vya kiarifu katika tungo za Kiswahili na lilikuwa na jumla ya alama 10.

Swali lilijibiwa na asilimia 51.5 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri ambapo watahiniwa wengi (81%) waliweza kupata alama 3.5 hadi 10. Kati yao, asilimia 60.4 walijibu vizuri na kupata alama 6 hadi 10. Katika majibu yao, baadhi ya watahiniwa waliojibu vizuri zaidi waliweza kutaja na kufafanua vipashio vya kiarifu kama vile; (i) *huundwa na kitenzi kikuu (ii) huundwa na kitenzi kishirikishi, (iii) huundwa na kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu (iv) huundwa na shamirisho (v) huundwa na chagizo* na kutoa mifano dhahiri. Watahiniwa wengine walitaja na kufafanua vipashio vya kiarifu bila mifano na hivyo kushindwa kupata alama zote. Kielelezo 5.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejitahidi kufafanua vipashio vya kiarifu na kutoa mifano kama swali lilivyoelekeza.

**Kielelezo 5.1**

5. Kiarifu: Ni sehemu ya sentensi ambayo hutoa taarifa iliyotendwa na mtenda ambaye huwa kiti shwa na Alama A

mfano - Mwalimu / anafundisha darasani
A

- Mwalimu / anaadhibu watoro
A

Zipeatazo ni Dondoo kuhusu vipashio ambavyo huunda kiarifu.

Shamirisho: Ni sehemu ya sentensi ambayo hukaliwa na kikundi Nomino upande wa kiarifu. Shamirisho huweza kuwa Nomino peke yake au Nomino na kivumishi

Mfano, Wanafunzi wanasoma / kitabu kizuri
KN

Chagizo: Ni sehemu ya sentensi katika upande wa kiarifu ambayo neno kuu huwa ni kielezi

mfano Mama ameenda / sokoni
E


a. Kitenzi kikuu, katika sehemu ya kiarifu huweza kukaliwa na kitenzi kikuu kimoja au zaidi

mfano Wanafunzi / wanasoma kitabu
T

Kitenzi kisaidizi: Ni aina ya kitenzi ambayo husaidia kitenzi kikuu. Kitenzi hiki kinaweza kukaa peke yake kimoja au zaidi ya kimoja

mfano. - Baba alikuwa analima
Ts

- Mwanafunzi alikuwa anataka kusoma
Ts T


5. Kitenzi kishirikishi, pia katika upande wa kiarifu huweza kuwakilishwa au kukaliwa na kitenzi kishirikishi ambacho ni: ndiye, si, ni na ndiye.
Mfano - Huyu ni mwalimu
t
- Juma ndiye aliyeleta kitabu
t
Hivyo basi kiarifu huundwa na vipashio mbalimbali ili kukamilisha usimilishi — ambao umeelezwa, vipashio hivyo ni shamirisho, chagizo, kitenzi kikuu, kitenzi kisaidizi na kitenzi kishirikishi.

Kielelezo 5.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyefafanua vipashio vya kiarifu na kutoa mifano kama jibu la swali lilivyotakiwa.

Asilimia 20.6 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani yaani 3.5 hadi 5.5 kutokana na kutoa baadhi ya hoja ambazo hazikujitosheleza katika majibu yao. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja kipashio kimojawapo kuwa ni chagizo lakini mifano aliyoitoa ilihusu vitenzi badala ya vielezi.

Aidha, watahiniwa wachache (19%) kati ya waliojibu swali hili walipata alama 0 hadi 3 ambazo ni chini ya kiwango cha wastani cha kufaulu. Watahiniwa hao walikosa maarifa kuhusu sehemu za tungo yaani *kiima* na *kiarifu*. Baadhi yao, walitaja na kufafanua aina za virai kama vile; *kirai nomino, kirai kivumishi, kirai kielezi, kirai kitenzi pamoja na kirai kiunganishi* badala ya kutaja na kufafanua vipashio vya kiarifu kama swali lilivyoulizwa. Watahiniwa wengine katika kundi hili walitaja vipashio vya kiima na vya kiarifu kwa pamoja, kinyume na matakwa ya swali. Kielelezo 5.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa kutaja aina za virai katika sentensi badala ya kutaja na kufafanua vipashio vya kiarifu.

**Kielelezo 5.2**

5 Kwanja ni sehemu ya sentensi au fungu ambayo huelezea au kuonesha utoshelevu wa fungu au sentensi hiyo. Kwa mfano

Mtoto anakula ugali. hapa kwanja ni anakula ugali.

Kuna vipashio mbalimbali vya kwanja katika fungu za Kiswahili mo ngoni mwa hizo ni hizo vifuatavyo

Kirai nomino hiki ni kipashio ambacho kazi yake kubwa katika kwanja ni kuonesha jinsi jina la kitu, mtu au mahali jinsi lilivyo tumika. Kwa mfano

Baba anakuja na ~~st~~ mama anapika

5 Hivyo neno "mama" katika kwanja limetumika kama kwanja.


Kirai kivumishi ni miongoni mwa vipashio ambavyo hutoa taarifa zaidi juu ya nomino. Hali hii hujitokeza katika kwanja kwa mfano.

Gari lile ni zuri sana
KV

Hivyo neno "zuri" limetumika kama kipashio katika kwanja.

Kirai kielezi ni vipashio ambavyo hutumika katika fungu kuonesha sehemu ambapo tendo au jambo fulani limefanyika au litafanyika. Kwa mfano shuleni, nyumbani na sehemu nyingine kwa mfano

Mtoto baada ya kupigwa alikimbia kuelekea shuleni
~~Kirai~~ KE



Kirai Kitenzi ni kipashio cha
kwanza ambacho hueleza jinsi ya
tendo lilivyofanyika, linavyofanyika na
litakavyofanyika kwa wakati [illegible]
huu.
Kwa mfano
Mjomba wangu anafuga mbuzi na
ng'ombe KT
Kirai kiunganishi ni kipashio
ambacho hutumika katika tungo
kwa kuunganisha sentensi mbili

Kielelezo 5.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa ambaye alieleza aina ya virai badala ya kueleza vipashio vya kiarifu katika tungo za Kiswahili.

### 2.2.7 Swali la 6: Utumizi wa Lugha

Swali lilitoka katika mada ya *Utumizi wa Lugha* na lilimtaka mtahiniwa kueleza faida tano na hasara tano za kutumia misimu katika lugha ya Kiswahili. Swali lililenga kupima tathmini na lilikuwa na jumla ya alama 10.

Swali lilijibiwa na asilimia 96.5 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Idadi kubwa ya watahiniwa hao (98.1%) walipata alama 3.5 hadi 10. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri zaidi. Kati ya watahiniwa hao, asilimia 72 walilijibu swali vizuri na kupata alama 6 hadi 10. Katika kundi hili, baadhi ya watahiniwa walijibu vizuri kwa kueleza faida tano na hasara tano za kutumia misimu katika lugha ya Kiswahili na kutoa mifano dhahiri. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika kwa usahihi faida za misimu kama vile; *kukuza lugha, kupamba lugha,* na *kuwa kitambulisho cha jamii*. Kwa upande wa hasara za misimu mtahiniwa aliandika; *Misimu ina chuku/chumvi nyingi, hutumia lugha ya matusi, huharibu lugha* na *hupunguza hadhira* na kuthibitisha kwa mifano sahihi. Watahiniwa wengine waliweza kuandika faida na hasara za misimu kwa usahihi lakini hawakuthibitisha hoja zao kwa mifano na hivyo kupata alama pungufu. Kielelezo 6.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kutoa mifano dhahiri.

**Kielelezo 6.1**

6.

Misimu ni Maneno yanayozushwa na Ki
kundi fulani cha watu wa jamii moja kuonyesha
umoja au uhusiano wao. Misimu huwera kuzuka
na na kupotea lakini kuna baadhi ya Maneno
ambayo ni Misimu huwera kusanifishwa na kuwa
lugha rasmi Mfano neno "Makabwela" ni ne
no lililozuka miaka ya 1980 likimanisha watu
wa tabaka la chini, maskini lakini limesanifishw
a na kuwa lugha au Msamiati

Hivyo basi Misimu inafaida nyingi
sana katika lugha ya Kiswahili kama ifuatavyo.

**Misimu** hukuza lugha ni kwa maana
kwamba misimu huwera kuongeza lugha kwa kuo
ngeza watumiaji na kuongeza eneo la utumiaji wa
lugha husika kwa kuongeza Misamiati amba
yo inaonyesha ukuaji wake.

Mfano kuna Maneno Mengi ya Kiswahi
li ambayo yametokana na misimu Mfano
Makabwela, walalahoi, arihi, msela.

**Misimu** hupamba lugha ni kwa kuo
ngeza mvuto unaomfanya mtu awere kupenda ku
tumia lugha husika, Misimu huongeza shauku
kwa mzungumzaji au Mtumiaji yeyote ambaye ana
fahamu msimu husika.

Mfano Mtu kutoka arusha

Vipi chali angu!

Poa ni vipi arihi

Hapo lazima Muhusika ashawishike katika
kutumia lugha hiyo kwani ina mvuto unavutia wa
tu kutoka Kaskazini.

6 Misimu ni kitambulisho cha jamii fulani, hapa namanisha kuwa Misimu hutambulisha jamii fulani kwa kuonyesha kuwa mtumiaji wake anatokea upande gani

Mfano : ni Mazungumzo ya watu hawa

Vipi yahee!

Poa vipi hali yako yahee!

Hapo unajua kabisa ni watu kutoka Pwani au Zanzibar au Tanga ndio wanaozungumza hivyo.

Misimu hupunguza ukali wa maneno, ni moja ya faida nyingine ya Misimu kwani hupunguza ukali wa Maneno kwa kuwepo maneno yenye hali ya tafsida ndani yake

Mfano. Mwajuma amefungasha

badala ya Mwajuma ana Makalio makubwa.

Misimu huficha Mada kuwa ya uficho kwa kupunguza hadhira na Mada hiyo kuwafikia walengwa husika tu bila kujali wengine waliokuwepo eneo husika.

Mfano mwajuma ana umeme

Badala Mwajuma ameathirika

Hapo siyo watu wote watakao elewa kuwa mwajuma ameathirika.

Kwa upande mwingine Misimu ina hasara zake pia kama ifuatavyo!

Misimu ina chuku/imetiwa chumvi nyingi, hapa ni kwa Maana kwamba Misimu huwa na Maneno Mengi Sana ambayo ni yale yasiyo kuwa na Maana. Misimu huweza kukuza Jambo kuwa kubwa sana.

Mfano "Milimkuta na Maburungutu-

8 ya Pesa"

Wakati mawerekana kala siyo hela nyingi hila ilo neno "Mabunungutu" linaonyesha Wingi ambao ni Mkubwa Sana

Misimu hupunguza hadhira/watu walak ao kuelewa ni moja ya hasara nyingine Kwani Misimu siyo kila kitu mtu asiyeitahamu ataweza kuelewa kuna baadhi ya Misimu ni vigumu Sana Kuweza kuelewa Kwani huwa inatumika eneo husika tu

Mfano Naomba ng'ora

akimaanisha: Naomba simu

Hila kwa mtu asiyefahamu Maana ya neno "ng'ora" ni vigumu kuelewa.


Misimu huaribu lugha Kwani hu pendwa na watu wengi na kufanya watu kusahau kutumia lugha sahihi.

Mfano mimi ni watu wanaishi ma eneo ya Kaskazini ni nadra sana kukuta watu wakitumia lugha Kama ipasavyo, Kwa wame sha badilishwa na Mazingira waliyomo.

Misimu huzuka na kutoweka hivyo husindwa kudumu na kuwa lugha sanifu hapa tunaona Kuwa Misimu huweza kuzuka kwa muda fulani na kisha kuweza kupotea eneo husika.

Mfano

Amefulia ikiwa na maana hana hela au amefilisika



6 Kwa ujumla Misimu huwa na kuli
ya faida na hasara kama tulivyoona lakini huwa
na chanzo chake kama kundi la watu
kuonda ndo lugha fasaha, wengine hupenda
kuonekana ni watu wanaojua lugha zaidi
kuliko wengine kwa kutumia Misimu husika

Kielelezo 6.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri kwa kueleza faida tano na hasara tano za kutumia misimu katika lugha ya Kiswahili.

Hata hivyo, asilimia 26.1 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani yaani 3.5 hadi 5.5 kutokana na kutoa majibu ambayo hayakujitosheleza. Aidha, majibu ya swali hili yalitakiwa kuthibitishwa kwa mifano zaidi lakini baadhi ya watahiniwa hao hawakutoa mifano dhahiri ya kuthibitisha misimu husika. Hali kadhalika, watahiniwa wengine waliorodhesha tu hoja bila kuzitolea maelezo ya kutosha.

Aidha, watahiniwa wachache (1.9%) pekee ndio waliojibu swali hili chini ya wastani na kupata alama 0 hadi 3. Hii ilitokana na baadhi ya watahiniwa kuwa na maarifa kidogo kuhusu faida na hasara za misimu katika lugha ya Kiswahili na hivyo kutoa hoja zisizo sahihi kwenye baadhi ya majibu yao. Watahiniwa wengine hawakulielewa swali na hivyo kuandika faida na hasara za misemo badala ya misimu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika kueleza faida za misimu alitoa hoja kama; *inasaidia kuongezeka kwa rejesta za lugha na kuleta changamoto katika uongeaji*. Kwa upande wa hasara za misimu mtahiniwa aliandika; *hupotosha maana ya lugha ya Kiswahili, huwasaidia wahalifu kufanya uhalifu ;* majibu ambayo hayakuwa sahihi. Kielelezo 6.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeorodhesha baadhi ya faida na hasara za misimu ambazo sio sahihi katika lugha ya Kiswahili.

**Kielelezo 6.2.**


6 FAIDA ZA MISIMU:
(a) Humfanya mtu

6 Misimu ni neno ambalo hutumika
kwa muda fulani na kwa maana
fulani. Zifuatazo ni faida za misimu
FAIDA:
(i) Humfanya mtu mwingine kutofahamu
kitu gani kinaongelewa mfano - Rejesta
ya Ngurumo unaweza ukaita kitimoto
wali bwecha n.k.
(ii) Inasaidia kuongezeka kwa rejesta za
lugha
(iii) Huleta changamoto katika uongea.
(iv) Humfunua mtu mwingine asijue
nini kimeongelewa.
(v) Hutunza siri kwa wakati fulani

HASARA
(i) Hupoteza maana ya lugha
(ii) Huleta changamoto katika lugha
ya kiswahili
(iii) Husaidia wahalifu kufanya
uhalifu.
(v)

Kielelezo 6.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyetoa hoja ambazo hazikujitosheleza katika kueleza faida na hasara za misimu katika Kiswahili.


## 2.3 SEHEMU C: UTUNGAJI

### 2.3.1 Swali la 7: Uandishi wa Insha

Swali lilihusu mada ya *Utungaji* katika kipengele cha uandishi wa insha. Swali lililenga kupima uundaji na lilimtaka mtahiniwa kuandika insha ya maneno yasiyopungua mia tatu na hamsini (350) na yasiyozidi mia nne (400) kuhusu ‘Mchango wa Vijana katika Maendeleo ya Taifa.’ Swali lilikuwa na jumla ya alama 20.

Swali lilijibiwa na watahiniwa wengi (99.6%) kati ya watahiniwa wote waliofanya mtihani kwa kuwa lilikuwa ni swali la lazima. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili na kufaulu kwao kiasilimia kumewasilishwa vizuri katika Chati Na. 3 kwa

kuonesha kufaulu kwa kiwango hafifu, kufaulu kwa kiwango cha wastani na kufaulu kwa kiwango kizuri.




**Chati Na. 3**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Asilimia 96.1 ya watahiniwa hao walipata alama 7 hadi 20 kwa kuwa waliweza kuandika insha kwa kuzingatia matakwa ya swali kwa viwango tofauti. Idadi kubwa ya watahiniwa hao (55%) walilijibu vizuri na kupata alama 12 hadi 20. Baadhi yao waliandika insha kwa usahihi zaidi kwa kuzingatia idadi ya maneno yasiyopungua mia tatu na hamsini (350) na yasiyozidi maneno mia nne (400) kuhusu 'Mchango wa Vijana katika Maendeleo ya Taifa.' Aidha, watahiniwa hao pia waliweza kuandika insha kwa kuzingatia; *kichwa cha insha kilichoandikwa kwa herufi kubwa, matumizi ya alama za uandishi, matumizi ya lugha sanifu, idadi ya maneno na upangaji wa mawazo kimantiki katika kufafanua mchango wa vijana katika maendeleo ya taifa.* Watahiniwa wengine waliopata alama za juu waliandika insha yenye upungufu katika idadi ya maneno au ongezeko la maneno kinyume na mahitaji ya swali hivyo kupata alama pungufu. Kielelezo 7.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeandika insha iliyokidhi vigezo vyote vilivyohitajika katika kujibu swali hili.

**Kielelezo 7.1**

07. MCHANGO WA VIJANA KATIKA MAENDELEO

Vijana ni rika ya watu wenye nguvu katika jamii. Maendeleo ni hatua ya kubadilika kutoka hali duni kwenda hali nzuri kimaisha, kiuchumi na kijamii. Vijana wanamchango mkubwa katika kujenga taifa kwa sababu wananguvu za kutasha. Vijana wameshiriki kuleta maendeleo katika taifa kama ifuatavyo.

Ujasiria mali, vijana wengi wamejiingiza katika ugunduzi na uwekezaji wa biashara ndogo ndogo, pia kazi tofauti tofauti zinazo wapatia kipato katika maisha yao na hata taifa kwa ujumla mfano. Wamachinga, washoni, wafugaji na wanamitindo hivyo wamesaidia kuongeza kipato kwa jamii na kulipa kodi katika taifa hali mayo maendeleo.

Masuala ya ulinzi, vijana wengi wamejiu-nga na jeshi la taifa (JKT), jeshi la wananchi (Jwt) pia wanamchango mkubwa katika kulinda amani ya nchi na usalama wa taifa. kwa uhalisia hata mgambo wengi wanapatikana kutoka kundi la vijana wenye umri wa miaka 18 mpaka 45. Hivyo kupitia ulinzi wao wa mali za umma wamsaidia kuleta maend-eleo katika taifa.

Shughuli za kilimo, vijana wana mchango mkubwa katika kilimo ambacho ndio uti wa mgongo wa taifa letu kwani wamejiingiza katika kilimo cha mazao na ufugaji hivyo wamesaidia kuongeza upati-kanaji wa chakula na mazao ya biashara.

07. Katika suala la elimu, vijana wengi ni wasomi hivyo wamechangia maendeleo katika jamii kwa kuongeza idadi kubwa ya wasomi na kuongeza wajuzi mbali mbali wanaotumiwa katika viwanda masuala ya sayansi na teknolojia, hivyo wamepunguza idadi ya wajinga na kuiendeleza elimu ya taifa letu katika ushindani duniani.

Mchango wa vijana katika uongozi. Vijana wengi wamejiingiza katika masuala ya siasa na uongozi wa jamii zetu mfano wabunge, madiwani, watendaji na wenyeviti wengi ni vijana chini ya miaka 45 hivyo wameweza kubadilisha mfumo wa uongozi na kwenda na wakati kulingana na matakwa ya vijana wengi hivyo wamehamasisha maendeleo katika siasa na demokrasia ya taifa.

Suala la Sanaa, Muziki na michezo ya taifa letu huendelezwa na vijana, mfano wasanii wa dini, bongo fleva, taarabu na ngoma za asili hubuniwa na vijana pia michezo ya mpira wa pete, riadha, ulondoa, na mipira ya wavu na miguu huchezwa na vijana walasiwa zoe mfano wa wasanii ni Diamondi, Mrisho mpoto. Kupitia wasanii hawa wameweza kutangaza tamaduni zetu Watanzania na kuendeleza utamaduni wetu.

Kwa ujumla vijana wanamchango mkubwa sana lakini pia wanakabiliwa na changamoto mbali mbali zinazokudisha


07 nyuma mipango yao, mfano hawana mitaji ya kutosha, wengi wamekosa ajira hivyo wanajiingiza katika uvutaji bangi na madawa ya kulevya, pia hawajapewa kipaumbele na taifa katika sanaa zao, mwisho vijana wapewe msaada na waweze shu kielemu ili walete maendeleo zaidi.


Kielelezo 7.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeandika insha nzuri kwa kuzingatia idadi ya maneno, matumizi ya lugha sanifu, taratibu za uandishi na mpangilio wa hoja wenye mantiki.

Hata hivyo, asilimia 41.1 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata alama za wastani yaani alama 7 hadi 11.5 kutokana na kuandika insha ambayo haikujitosheleza kwa baadhi ya vigezo muhimu vya uandishi wa insha. Watahiniwa hao, waliandika insha kwa kuzingatia vigezo vichache na kutoa ufafanuzi usiokuwa dhahiri kuhusu ‘Mchango wa Vijana katika Maendeleo ya Taifa.’

Aidha, asilimia 3.9 pekee ya watahiniwa waliofanya swali hili hawakujibu kwa usahihi na hivyo kupata alama chini ya wastani yaani alama 0 hadi alama 6.5 kutokana na kuandika insha isiyokidhi viwango vya uandishi wa insha. Baadhi ya watahiniwa hao, hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu vigezo muhimu vya kuzingatia katika uandishi wa insha kama vile idadi ya maneno, matumizi ya lugha sanifu na mpangilio wa hoja wenye mantiki na hivyo kupata alama za chini. Kielelezo 7.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyetunga hadithi kuhusu mchango wa vijana katika maendeleo ya taifa kinyume na matakwa ya swali.

**Kielelezo 7.2**


7. Vijana, Vijana, Vijana ni nguvu ya Taifa lolote
na hasa hili la leo na Vijana wote ni tegemeo
la kizazi cha Wazee na watu wanakuja. Ni
ninaposema hivyo ni kumbuka wewe kijana mwenye
Miaka kumi na minane hadi miaka thelathini
na tano na hata arobaini na mitano sasa
wewe ni kijana unategemewa na taifa na
dunia yako kwa ujumla. Leo unayo nafasi
ya kuzungumza na vijana wote ya nchi hii
kote ya Tanzania na hata dunia kwa ujumla.


7. Nigeli penda kuma nianze na simulizi yangu hii
ya kaiwa Palikuwepo na Mfalme mmoja hivi
ambaye huyu yeye alipatikana huko nchi
za mbali. Mfalme huyu alikuwa na miaka
kumi na tisa na alifanikiwa kuwa madarakani
baada ya Baba yake kufariki. Mfalme huyu
kafanya mengi hata katika vazi kwa kufufua
vyuo vya Bambuzi na hata mwindo kibinu
mingine. Na kushindana na Mataifa makubwa
kivita, Na watu wake walimpenda sana hii
yote ni kwa sababu anapenda maendeleo chanya
Nawaasa vijana wenzangu kuwa hili
Taifa hili liendelee ni mpaka nguvu zetu.
kwa nguvu zote tunatoka sasa ni kujitu-
mea, kuacha uzembe, kuonyesha uzalendo
kwa ya kusaidia umoja na mshikamano
miongoni mwa sisi kwa sisi. ndipo tutafanikiwa
kwa hilo kama nchi ya Mfalme huyu
kijana alivyofanikiwa kwa haraka zaidi.
Pia vijana elimu tunatakiwa kuipu-
ata kwani ndicho chanzo cha maarifa kwa
kuchukua vitu vizuri na vya maendeleo
ndani ya jamii yetu.
Hata hivyo vijana kwa kuacha mambo
mabovu kama uvutaji bangi, madawa ya
kulevya si chanzo cha kushinda maisha
ni mpaka hata wazee na serikali kuwa
kwa undani zaidi kwa kutoa mawazo na
mtaji wa vijana hao hivyo tunu na
Taifa kwa ujumla litaendelea.


Kielelezo 7.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyetunga hadithi inayowausia vijana kuwa wema na kuepuka uvutaji wa bangi na madawa ya kulevya badala ya kuandika insha kuhusu mchango wa vijana kwa taifa.

## 2.4 SEHEMU D: MAENDELEO YA KISWAHILI

### 2.4.1 Swali la 8: Usanifishaji

Swali lilihusu mada ya *Maendeleo ya Kiswahili* katika mada ndogo ya *Usanifishaji wa Lugha ya Kiswahili*. Swali lilimtaka mtahiniwa kuelezea matukio saba muhimu yaliyofanywa na serikali za Tanganyika na Zanzibar katika harakati za kusanifisha lugha ya Kiswahili kabla ya mwaka 1960. Swali lililenga kupima maarifa na lilikuwa na jumla ya alama 20.

Swali lilijibiwa na asilimia 44.5 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili na kufaulu kwao kiasilimia kumefafanuliwa vizuri katika Chati Na.4 kwa kuonesha kufaulu kwa kiwango hafifu, kufaulu wa kwa kiwango cha wastani na kufaulu kwa kiwango kizuri.




**Chati Na. 4**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Asilimia 95.6 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 7 hadi 20 kutokana na maarifa waliyokuwa nayo kuhusu usanifishaji wa lugha ya Kiswahili. Kati yao, watahiniwa wengi (81.2%) walilijibu vizuri na kupata alama 12 hadi 20. Watahiniwa hao kwa viwango tofauti waliweza kueleza matukio saba muhimu ya usanifishaji wa Kiswahili kabla ya mwaka 1960 yaliyofanywa na serikali za Tanganyika na Zanzibar kama vile ; *Mwaka 1925 – Mkutano wa kuchagua lahaja itakayotumika katika shule za Afrika ya Mashariki. Mwaka 1928 – Kuteua lahaja ya kiunguja ili itumike katika shughuli zote rasmi katika*

*Afrika ya Mashariki*. Kielelezo 8.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kueleza matukio saba muhimu ya usanifishaji kabla ya miaka ya 1960 yaliyofanywa na serikali za Tanganyika na Zanzibar.

**Kielelezo 8.1**

8. Kusanifisha ni hali ya kusawazisha mai tofauti zilizomo ndani ya wazungumzaji wa Lugha moja. Katika kusanifisha hatua zifuatazo sharti zipitiwe mfano kuteua Lahaja ya usanifishaji kuandwa kwa chombo cha usanifishaji na vile vile kuhakikisha matamshi na kuandaa wataalam na kamusi. Hivyo basi Lugha ya Kiswahili ilisani-fiwa chini ya utawala wa Mwingereza kwa malengo ya kutumika katika shughuli za ngazi za chini na mashuleni yaani darasa la kwanza mpaka darasa la nne (I — IV). Hivyo basi yafuatayo ni matukio yaliyofanywa na serikali ya Tanganyika na Zanzibar katika harakati za kusanifisha Lugha ya Kiswahili kabla ya miaka 1960.

Kuitishwa kikao na Gavana Donald Cameroon mwaka 1925 mjini Dar es Salaam na kazikutanisha nchi zote nne za Afrika mashariki Lengo likiwa ni kutafuta Lugha ambayo ingeweza kutumika mashuleni. Wakati huo Lugha za kikabila Kiingereza na Kiswahili cha kilahaja ndizo zilizo-tumika mashuleni na hata katika shughuli za kiutawala hasa ngazi za chini. Hivyo basi hili ndilo tukio la kwanza katika harakati za kusanifisha Lugha ya Kiswahili kabla ya miaka ya 1960

Mwaka 1928 Lahaja ya Kiunguja ilichaguliwa kuwa ndio Lahaja ya usanifishaji na kuiacha Lahaja ya Kingozi ilivyokuwa ina pigiwa upato mkubwa. Lahaja hiyo ya Kiunguja ilikubaliwa huko Mombasa ili iweze kusanifiwa na kuwa Kiswahili fasaha kutokana na sifa mbalimbali kama vile kuwa na msamiati wa

8 kutosha, kuendana na utawala uliokuwepo na hata
hivyo ilikuwa imeenea sehemu kubwa na hivyo
kuteuliwa kama lahaja ya usanifishaji. Hivyo basi
kuteuliwa kwa lahaja kiunguja kutoka Zanzibar
lilikuwa tukio la pili katika harakati za usanifishaji
lugha ya kiswahili kabla ya miaka ya 1960.

Mwaka 1930 iliundwa kamati ya
usanifishaji Afrika mashariki iliyoitwa "The inter-
territorial swahili Language committee" na Profesa
Carl Meinhof akiwa kama mshauri. Kamati hii
ilikuwa na lengo la kukuza matumizi sanifu ya
kiswahili na kuwashauri waandishi chipukizi na
kuwatia moyo. Kamati ya kiswahili Afrika mashariki
ilifanikiwa kutoa majarida mbalimbali na hata
kamusi mfano "~~Eng~~ "standard English-swahili
Dictionary na "standard swahili-English Dictionary
Hili ndilo lilikuwa tukio la tatu katika harakati
za usanifishaji wa kiswahili kabla ya miaka ya 1960

1948 Tukio lililofuata lilikuwa ni kuundwa
kwa shirika la uchapaji wa miswaada lililoitwa
"East Africa Literature Bureau" lililoshughuli-
sha na uchapaji wa miswaada, kuwatia moyo
waandishi chipukizi na hata kutoa majarida
mbalimbali. Katika hatua nyingine "East Afrika
Literature Bureau lilitoa vitabu kama vile
"Dialects of swahili". Hivyo basi hili ndilo lilikuwa
tukio la nne katika harakati za usanifishaji
wa lugha ya kiswahili kabla ya 1960.

1952 Tukio lililofuata lilikuwa ni kuweka
kamati ya lugha ya Afrika mashariki
"The inter-territorial swahili Language Committee"
chini ya chuo kikuu cha Afrika mashariki

8 cha Makerere kilichopo nchini Uganda ilikuwa
mwaka ~~1948~~ 1952 katika taasisi ya "Institute of social
research" - katika hali hiyo shughuli za taasisi
hiyo zilipanuka na kuanza kachunguza lahaja
nyingine mbalimbali kama vile lahaja ya kimvita,
lahaja ya kingozi, kipate n-k - Hivyo basi hili
ndilo lilikuwa tukio la tano katika harakati
za usanifishaji wa lugha ya kiswahili

Tukio lililofuata lilikuwa ni kujito
keza kwa vyombo mbalimbali vya habari kama
vile Radio na Magazeti yaliyoibuka na kuanza
kutumia kiswahili sanifu - Radio kama vile
Radio Dar es salaam au sauti ya Dar es salaam
Radio Pwani n-k na pia magazeti mbalimbali
kama vile Kiongozi yaliibuka na kuanza
kutumia kiswahili sanifu katika habari za
redioni na Magazeti kama vile kipindi cha
sauti ya Bagamoyo kilisaidia kueneza matumizi
sanifu ya kiswahili, na hivyo kuelezea moja
ya matukio katika harakati za usanifishaji
wa kiswahili kabla ya miaka ya 1960.

Mwaka 1959 "UKUTA" (usanifu wa
kiswahili na ushairi Tanganyika) iliundwa
malengo ya kuwatia moja waandishi na
kuwapa ushauri, na pia kuendesha semina
fupi fupi za kiswahili na pia UKUTA
waliendesha mashindano ya uandishi wa
mashairi na mwisho walito majarida mbali-
mbali ya kiswahili - Hivyo hii ndio ikawa
hatua ya saba na ya mwisho katika
usanifishaji wa kiswahili chini ya waingereza
kabla ya miaka ya 1960.

Kielelezo 8.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri ingawa katika majibu yake kulikuwa na kosa la kitahijia kama : kuwatia moja’’ badala ya ‘‘kuwatia moyo’’na kosa la upatanisho wa kisarufi kwa kuandika ‘‘chache’’ badala ya ‘‘vichache.’’ Pia mtahiniwa hakutoa hitimisho.

Aidha, asilimia 14.4 ya watahiniwa waliojibu swali hili, walipata alama za wastani yaani alama 7 hadi 11.5 kutokana na kushindwa kueleza matukio na wakati wake muafaka. Aidha, baadhi yao walitoa maana ya usanifishaji ambayo haikuwa sahihi na wengine walichanganya miaka/wakati wa tukio fulani na kutoa maelezo ambayo hayakujitosheleza katika kuelezea matukio hayo.

Hata hivyo, watahiniwa wachache sana (4.4%) walipata alama chini ya wastani yaani alama 0 hadi 6.5 kutokana na kutoa majibu yasiyokidhi matakwa ya swali. Baadhi ya watahiniwa hao, walieleza mambo yanayosaidia kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili kama vile; *Elimu, Utawala, Dini, Mashamba, Jeshi la K.A.R, Vyombo vya habari na kampeni za kisiasa* badala ya kueleza matukio saba ya usanifishaji yaliyofanywa na serikali ya Tanganyika na Zanzibar kabla ya 1960. Watahiniwa wengine walitoa majibu yasiyohusiana kabisa na dhana ya usanifishaji wa lugha ya Kiswahili na hivyo kupata alama 0. Kielelezo 8.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeeleza mambo yanayosaidia kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili kinyume na matakwa ya swali.

**Kielelezo 8.2.**

SEHEMU D

8 Usanifishaji ni hali ya kuifanya lugha ikubalike na itumike na jamii nzima inayozungumza lugha hiyo. Katika kusanifisha lugha ya kiswahili Serikali ya Tanganyika na Zanzibari ilitumia njia mbali mbali ili kuifanya kiswahili kikubalike na kutumia nazo ni.

Elimu. Katika Serikali ya Tanganyika na Zanzibari kabla ya miaka ya 1960 ilikuwa chini ya utawala wakikoloni ambao ni Waingereza. Nawa walitumia lugha ya kiswahili kama lugha ya mawasiliano kuanzia darasa la kwanza hadi la nne na kama somo kuanzia la nne hadi la kumi na mbili na kuifanya ikubalike.

Utawala. Waingereza au Serikali ya Tanganyika na Zanzibari ilikuwa na utawala wa kikoloni ambapo walilazimisha kila chifu ajue kiswahili ili kurahisisha utawala na lugha ya kiswahili ilikuwa ndio lugha ya mawasiliano.

Dini. Serikali ya Tanganyika na Zanzibari kabla ya miaka ya 1960 walitumia dini kama kigezo cha kukuza na kueneza lugha ya kiswahili kwa kutoa mahubiri na mawaidha na lugha ya kiswahili ndio ilikuwa lugha ya mawasiliano.

Mashamba. Serikali katika miaka hiyo walianzisha mashamba makubwa ya mkonge na walichukua watu kutoka sehemu mbali mbali na kufanya kazi katika mashamba yale lugha iliyotumika ilikuwa kiswahili

Jeshi la KAR Hili ni jeshi lililokuwa linapigania uhuru mbozi wa bara la Afrika na katika kila sehemu

waliyepita walitumia lugha ya Kiswahili na kuifanya ikubalike na kutumika.

Vyombo vya habari vilisaidia lugha kuweza kusanifishwa. Vyombo vya habari kama magazeti radio vilitumia lugha ya Kiswahili kufikisha habari katika jamii na kuifanya ikubalike vyombo vya habari ni kama RTD Radio Tanganyika Dar es Salaam magazeti kama habari leo Sauti ya pwani.

Kampeni za kisiasa zilizofanywa na wanaharakati katika ya kulikomboa bara la Afrika. Baada ya vita vya pili vya dunia mataifa mengi ya Kiafrika kama Tanganyika walifanya kampeni za kisiasa ili kuondoa ukoloni na walitumia lugha ya Kiswahili na kuifanya ikue na kukubalika na jamii ya watu wengi

Tunaweza kuhitimisha kwa kusema kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili nchini Tanzania ni katika kipindi na juhudi za wakoloni walitumia lugha ya Kiswahili - katika nyanja mbali mbali na kuifanya kuenea sehemu kubwa ya nchi

Kielelezo 8.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kuelezea matukio saba ya usanifishaji yaliyofanywa na serikali ya Tanganyika na Zanzibar kabla ya 1960.

### 2.4.2 Swali la 9: Kukua na Kuenea kwa Kiswahili

Swali lilihusu mada ya *Maendeleo ya Kiswahili* katika mada ndogo ya *Kukua na Kuenea kwa Kiswahili baada ya Uhuru*. Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza hoja tano zinazoonesha jinsi serikali ya Tanzania inavyojizatiti katika kukinusuru Kiswahili dhidi ya kasumba zinazokikabili katika ukuaji wake. Swali hili lililenga kupima tathmini na lilikuwa na jumla alama 20.

Swali lilijibiwa na asilimia 55.1 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Miongoni mwa watahiniwa hao, asilimia 95.6 walipata alama 7 hadi 19.5 ambapo kati yao, asilimia 58.3 walilijibu vizuri na kupata alama 12 hadi 19.5. Baadhi ya watahiniwa hao waliopata alama za juu walieleza hoja zinazoonesha jinsi serikali ya Tanzania inavyojizatiti katika kukinusuru Kiswahili dhidi ya kasumba zinazokikabili katika ukuaji wake. Kwa mfano, mtahiniwa aliyefanya vizuri alieleza hoja kama vile; *kuundwa kwa taasisi mbalimbali zinazoshughulikia ukuaji wa Kiswahili, Kiswahili kutumika katika vyombo vya habari, Kiswahili kutumika kama lugha ya kufundishia elimu ya msingi* na kadhalika. Kwa upande wa hitimisho aliweza kutoa hitimisho zuri linaloendana na swali. Kielelezo 9.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

**Kielelezo 9.1.**

9. Kiswahili ni moja ya lugha amb-
ayo inazungumzwa Afrika Mashariki na Kati
pia Kiswahili ni lugha ya Taifa la Tanza-
nia na pia ni lugha rasmi ya taifa hilo
pamoja na mataifa mengine ya Afrika Ma-
shariki. Serikali ya Tanzania inafanya
juhudi kubwa kuhakikisha kuwa inakinusuru
Kiswahili dhidi ya kasumba zinazokikabili
katika ukuaji wake (kuongezeka kwa misa-
miati ya lugha hiyo) Zifuatazo ni hatua
ambazo Serikali ya Tanzania inazichukua
katika kunusuru lugha ya Kiswahili.

Kuruhusu kuundwa kwa taasisi
~~Taasisi~~ mbalimbali ambazo zinajishughulisha na
uchunguzi na ukuzaji wa Kiswahili mfano BAKITA
(Baraza la Kiswahili la Taifa)(TUKI) Taasisi ya
uchunguzi wa Kiswahili na taasisi nyinginezo
ambazo husaidia kukua na kuenea kwa
Kiswahili nchini Tanzania.

Kuruhusu Kiswahili kitumike kati-
ka vyombo vya habari ndani na nje ya nchi
~~ampa~~ ambapo watazamaji na wasikilizaji hupa-
ta matangazo kwa lugha ya Kiswahili mfano
wa vyombo vya habari vya kimataifa ni kama
vile BBC, VOA na vinginevyo pia vyombo vya
habari vya nchini Tanzania ni kama vile
TBC,, ITV, EATV, Radio One, Clouds na
vyombo vya habari vingine.

Kuruhusu Kiswahili kitumike
kama lugha ya kufundishia kwa elimu ya
msingi katika shule zote za Serikali na
kuweka somo la Kiswahili kuanzia elimu

9. ya msingi mpaka vyuo vikuu, hivyo kuli-
fanya Kiswahili kikue na kuongeza watu-
miaji wake, hivyo Kiswahili kinakua japo-
kuwa kinakumbwa na changamoto kadha wa
kadha.

Kuruhusu kitumike katika shughuli
maalum za kiserikali mfano Kiswahili kina
tumika Bungeni, kinatumika kwenye mikutano
ya kisiasa hivyo utumizi huo unakifanya
kikue na kuenea sehemu mbalimbali za
Tanzania na nje ya mipaka ya Tanzania.

Kuruhusu Kiswahili kitumike
katika shughuli za maendeleo kama
vile biashara hii inatokana na kitendo
cha serikali kukubali lugha ya Kiswahili
iwe lugha ya taifa la Tanzania hivyo
kimeongeza watumiaji na kukifanya kikue.

Mwisho lugha ya Kiswahili pamo-
ja na kukumbwa na changamoto katika
ukuaji wake bado kinaendelea kukua na
kuenea sehemu mbalimbali ulimwenguni kw-
a kuwa kinatumika katika sanaa mfano
katika muziki mwanamziki Miriam Makeba
wa Afrika Kusini aliimba kwa Kiswahili
wimbo uitwao Malaika. Pia katika filamu
Mwanadada Anjelina Jolie katika filamu
yake ya Tomb Rider anaongea Kiswahili
hivyo vote ni vithibitisho kwa Kiswahili
kinakua licha ya kukumbwa na kasumba
mbalimbali.

Kielelezo 9.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeeleza vizuri hoja zinazoonesha jinsi serikali ya Tanzania inavyojizatiti kukabiliana na kasumba zinazoikabili lugha ya Kiswahili.


Hata hivyo, asilimia 37.3 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani yaani alama 7 hadi 11.5 kutokana na kutoa hoja ambazo hazikujitosheleza. Pia, watahiniwa hao walitaja hoja bila kutoa ufafanuzi na mifano ya kukidhi majibu yaliyotarajiwa.

Aidha, asilimia 4.4 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama chini ya wastani yaani alama 0 hadi 6.5 kutokana na kutokulielewa vyema swali na kutoa majibu yasiyokidhi matakwa ya swali. Baadhi yao walieleza matatizo mbalimbali yanayoikabili lugha ya Kiswahili kama vile; *uhaba wa wataalamu wa lugha, sera ya wasomi kulegalega, uhaba wa fedha, ukosefu wa vifaa vya kufanyia kazi katika kukuza na kueneza lugha na ukosefu wa uzalendo katika lugha ya Kiswahili* badala ya kuelezea jinsi serikali ya Tanzania inavyojizatiti katika kukinusuru Kiswahili dhidi ya kasumba zinazokikabili katika ukuaji wake. Watahiniwa wengine walieleza sababu za kukua na kuenea kwa Kiswahili kama mkakati wa kunusuru lugha ya Kiswahili dhidi ya kasumba zinazoikabili kinyume na matakwa ya swali na hivyo kupata alama za chini. Kielelezo 9.2 ni mfano wa jibu la mtahiniwa aliyeeleza matatizo yanayokabili ukuaji wa lugha ya Kiswahili badala ya kueleza mikakati ya kunusuru Kiswahili dhidi ya kasumba mbalimbali zinazokabili ukuaji wake.

**Kielelezo 9.2**

9. Kiswahili, Ni mchangamyiko wa lugha mbali mbali utokanao na Lugha za kibantu. Hoja tano nikionesha jinsi Serikali ya Tanzania inayojizatiti kukinusuru kiswahili dhidi ya ukasumba zinazokikabili katika ukuaji wake ni kama vile:-

Uhaba wa Wataalamu wa Lugha, kutokana na uhaba au upungufu wa wataalamu hupelekea kukinusuru kiswahili dhidi ya kasumba zinazokikabili katika ukuaji wake. Mfano Serikali kutotoa msaada wa kuwasomesha wataalamu hao, kutotoa Mikopo ya kutosha kwa wanaosoma lugha hiyo na hivyo kukinusuru kiswahili.


9. Sera ya Wasomi kulegalega;- baadhi ya Wasomi kukisaliti Kiswahili kutokana na Wasomi kupata ajira nje ya nchi mfano,' baadhi ya wataalamu kuchukuliwa kwenda kufundisha nje ya nchi kama vile, Marekani, Kenya, Uganda na Rwanda na hivyo kiswahili kukinusuru dhidi ya Ukasumba zinazokikabili katika ukuaji wake.

Uhaba wa fedha;- kupitia uhaba wa fedha kwa ajili ya kuchapisha vitabu, kamusi, na majarida mbalimbali, kumepelekea kukinusuru kiswahili dhidi ya kasumba zinazokikabili katika ukuaji wake.

Ukosefu wa vifaa vya kufanyia kazi katika kukuza na kukieneza zaidi mfano, kama vile, kompyuta, vitabu mbalimbali vya kuweza kukuza na kuinua kiswahili na hivyo hupelekea kukinusuru kiswahili dhidi ya kasumba zinazokikabili katika ukuaji wake.

Ukosefu wa Uzalendo katika lugha ya kiswahili;- kutokana na ukosefu wa uzalendo kumechangia sana baadhi ya Wasomi kujikana wenyewe katika utumiaji wa Lugha ya kiswahili na hivyo kupelekea kujizatiti kukinusuru kiswahili dhidi ya kasumba zinazokikabili katika ukuaji wake.

Kwa hiyo basi, Wasomi na Watanzania wote si budi kuwa Wazalendo na lugha yetu pia Serikali iwekeze fungu ya kiswahili ili kuweza kukikuza zaidi nchini.

Kielelezo 9.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeeleza matatizo yanayokabili ukuaji wa lugha ya Kiswahili kinyume na matakwa ya swali.


## 2.5 SEHEMU E: TAFSIRI

### 2.5.1 Swali la 10: Nadharia ya Tafsiri

Swali lilihusu mada ya *Tafsiri* na lilimtaka mtahiniwa kuthibitisha kauli isemayo utoshelevu wa tafsiri hutokana na

mfasiri mwenyewe na kisha kutoa sababu nne zinazomfanya mfasiri kupata tafsiri toshelevu. Swali hili lililenga kupima maarifa na lilikuwa na jumla ya alama 20.

Swali lilijibiwa na watahiniwa wengi (99.3%) kati ya watahiniwa wote waliofanya mtihani kwa kuwa lilikuwa ni swali la lazima. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili na kufaulu kwao kiasilimia kumewasilishwa vizuri katika Chati Na.5 kwa kuonesha kufaulu kwa kiwango hafifu, kufaulu kwa kiwango cha wastani na kufaulu kwa kiwango kizuri.




**Chati Na. 5**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Asilimia 66.2 ya watahiniwa hao walipata alama 7 hadi 18. Aidha, watahiniwa wachache, (14.1%) tu ndio waliofanya vizuri na kupata alama 12 hadi 18 kutokana na kuweza kuthibitisha kauli isemayo, 'Utoshelevu wa tafsiri hutokana na mfasiri mwenyewe' na kutoa sababu nne zinazomfanya mfasiri kupata tafsiri toshelevu'. Hoja madhubuti zilizotolewa na baadhi ya watahiniwa hao ni kama vile; *mfasiri anapaswa kufahamu lugha zote mbili, kuzingatia weledi wa wasomaji, kujua misingi ya tafsiri yake, kuwa mjuzi na mpana wa habari.* Vilevile watahiniwa wengine waliweza kutoa hoja sahihi zenye utangulizi mzuri na hitimisho linaloendana na swali. Kielelezo 10.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri kwa kutoa sababu nne zinazomfanya mfasiri kupata tafsiri toshelevu.

## Kielelezo 10.1


10 ~~ut~~ Tafsiri ni kitendo cha kuhawilishaji kutoka
mawazo katika lugha chanzi kwenda lengwa
kwa njia ya Maandishi wakati mfasiri ni
mtu anayetafsiri kazi hiyo. ~~tupo~~ Ni kweli kwamba
utoshelevu wa tafsiri hutokana na mfasiri mwenye
-we kwa sababu zifuatazo:-

Mfasiri anapaswa afahamu lugha zote mbili
kinagaubaga, ili mfasiri apate tafsiri toshelevu
lazima afahamu lugha zote mbili chanzi na lengwa
kimsamiati, kimaana, kimuundo na sehemu
husika lugha hiyo hutumika pia mfasiri
aboini Msamiati kwa kuangalia istilahi tofauti
za kupata Maana kamili ya kimawasiliano.

Mfasiri anapaswa Azingatie weledi na
wasikilizaji na pia wasomaji, Mfasiri ili kazi
yake iwe toshelevu lazima azingatie weledi na
wasomaji wa kazi yake ya tafsiri kwa sababu
ndio walengwa hivyo anapaswa kuzingatia
lugha inayoeleweka na weledi wake ili tafsiri
yake iweze kujitosheleza mfano Tanzania tunatumia
kiswahili sana hivyo tafsiri yake aweke katika
Lugha ya kiswahili inayoeleweka kwa urahisi

Tatu mfasiri anapaswa kujua Misingi ya
tafsiri yake, Mfasiri anapaswa kujua kazi
yake kuu ni kutafsiri hivyo anapaswa kuzingati
-a misingi hiyo kama vile kutoa mawazo
yake hiyo siyo kazi yake katika tafsiri hivyo
kazi yake inaweza kujitosheleza.

Nne mfasiri anapaswa awe mjuzi wa
mpana wa habari, Mfasiri anapaswa aelewe
mambo yanayotokea na kutokea katika jamii
mbalimbali ili kuweza kupata uhalali wa uelewa



10 zaidi ya kile anachokitafsiri hii itampa kazi yake kuwa inajitosheleza na kueleweka kwa wasikilizaji zaidi.
Hivyo Nawaza kusoma kwamba ili mfasiri kupata utoshelevu katika kazi yake ni lazima kuzingatia zaidi lugha zote mbili na kuzitendea haki ipasavyo ili kuondoa Migogoro na kupata tafsiri ambayo ni toshelevu.

Kielelezo 10.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri ijapokuwa katika baadhi ya hoja zake alichanganya dhana ya tafsiri na ukalimani. Kwa mfano, katika hoja ya pili aliandika neno ‘‘wasikilizaji’’ neno linalotumika katika dhana ya ukalimani.

Hata hivyo, watahiniwa wengi (52.1%) waliojibu swali hili walipata alama za wastani ambazo ni alama 7 hadi 11.5 kutokana na kutoa majibu ambayo hayakuwa na ufafanuzi toshelevu kwa baadhi ya hoja ambapo wengine walichanganya dhana ya tafsiri na ukalimani katika majibu yao.

Aidha, asilimia 33.8 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama chini ya wastani yaani alama 0 hadi 6.5. Miongoni mwao, asilimia 1.1 walishindwa kujibu kwa usahihi na kupata alama 0 kutokana na kukosa maarifa juu ya dhana nzima ya tafsiri. Baadhi ya watahiniwa hao walieleza mchakato wa kutafsiri matini kama; *(i) Maandalizi, (ii) kuidurusu kazi , (iii) kusomwa na mtu mwingine, (iv) kuitoa kwa watu husika*, badala ya kutoa sababu nne zinazomfanya mfasiri kupata tafsiri toshelevu. Watahiniwa wengine walishindwa kutoa utangulizi na hitimisho linaloendana na swali na hivyo kupata alama chini ya wastani. Kielelezo 10.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeelezea mchakato wa kutafsiri matini asilia badala ya kueleza sababu nne zinazomfanya mfasiri kupata tafsiri toshelevu.

**Kielelezo 10.2**


10. i). Maandalizi. Kitu cha kwanza mfasiri lazima awe na maandalizi ya kutosha katika kazi yake. Anatakiwa kuangalia vifaa ambavyo anatakiwa kwa navyo katika kuikamilisha kazi yake.

10. ii) Kuirudusu kazi yake. Baada ya kufanya maandalizi mfasiri anatakiwa kuanza kuifanya kazi ya kutafsiri kazi yake yote

iii). Kuipeleka kwa wataalamu kwa ajili ya kuhakikiwa. Baada ya kuitafsiri

iii). Kuisoma na mtu mwingine. Baada ya kuitafsiri kazi yake anatakiwa aisome na mtu mwingine ili kuangalia mapungufu na kuyafanyia marekebisho.

iv). Kutoa kwa watu husika. Baada ya kuhakiki na kuirekebisha kazi yake mfasiri kutoa kazi yake kwa walengwa ili kupeleka ujumbe ulio kusudiwa.

Kielelezo 10.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutoa sababu nne zinazomfanya mfasiri kupata tafsiri toshelevu.

# 3.0 SEHEMU YA II: MTIHANI WA KISWAHILI KARATASI YA PILI

## 3.1 TATHMINI KWA KILA SWALI

## 3.2 SEHEMU A: FASIHI KWA UJUMLA

### 3.2.1 Swali la 1: Fasihi kwa Ujumla

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi kwa Ujumla* na lililenga kupima majazi ya utambuzi kuhusu uchambuzi. Swali hili lilimtaka mtahiniwa kufafanua kwa mifano mambo manne muhimu yanayoweza kumfanya mwandishi wa kazi za fasihi kuwa huru katika kuitetea na kuisemea jamii yake kuhusu matatizo mbalimbali yaliyopo bila kikwazo. Swali lilikuwa na jumla ya alama 20.

Swali lilijibiwa na watahiniwa wachache (28%) kati ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Hata hivyo, asilimia 87.6 ya watahiniwa hao walipata alama 7 hadi 19.5 ambapo miongoni mwao asilimia 72.1 walifanya vizuri na kupata alama 12 hadi 19.5 kwa sababu waliweza kufafanua mambo yanayomfanya mwandishi wa fasihi kuwa huru katika kuitetea jamii katika viwango tofauti. Baadhi ya watahiniwa hao waliweza kueleza mambo manne kama vile; *Uhuru wa mwandishi unavyoonekana katika utashi wake, jinsi ya kuitawala vema sanaa yake, lugha anayoitumia, falsafa inayoeleweka na kutoa hitimisho linalosadifu vizuri yale aliyoyazungumzia.* Aidha, watahiniwa wengine waliopata alama za juu hawakuweza kutaja mambo yote ingawa waliweza kutoa ufafanuzi toshelevu. Kielelezo 1.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu vizuri kwa kutoa mifano maridhawa.

**Kielelezo 1.1**

1\. Mwandishi ni mtu yeyote atumiaye muda wake kufikisha ujumbe kwa jamii kwa njia ya maandishi. Uhuru wa mwandishi ni hali ya mwandishi kuwa huru kuandika kazi yake kwa kuelimisha jamii, kuikosoa jamii, kukosoa tabaka tawala linaloenda kinyume na maadili bila kupingwa na tabaka lolote. Yafuatayo ni mambo muhimu yanayofanya ~~jamii~~ mwandishi wa kazi ya fasihi kuwa huru;

Uhuru wa mwandishi umo katika utashi; ili mwandishi awe huru ni lazima awe na utashi katika kuwasilisha kazi yake, asikubali kuyumbishwa na makombora ya watu wengine mwandishi mwenye utashi makombora kutoka kwa watu wengine yanamkomaza. Mfano wa mwandishi mwenye utashi ni NGUNGI WA THIONG

Uhuru wa mwandishi umo katika kutawala vyema sanaa yake; mwandishi anapaswa kutawala vyema sanaa yake ili kufanya kazi yake kuwa bora, mfano mwandishi anapaswa kuwa na ubunifu lakini ubunifu huo usizidi sana katika kazi yake pia asiegemee sana katika uhalisia kwani itamfanya kazi yake izuiliwe na tabaka tawala mfano riwaya ya Erick Shigongo (Rais anampenda mke wangu) imefungiwa kwa kuwa aliegemea sana katika uhalisia.

Uhuru wa mwandishi umo katika lugha anayotumia; mwandishi wa kazi ya fasihi anapaswa kutumia lugha ambayo inaeleweka katika jamii, vilevile anapaswa kutumia lugha yenye taswira, tamathali za semi na mambo mengine

Uhuru wa mwandishi umo katika falsafa inayoeleweka; mwandishi anapaswa kuwa na imani ambayo inaeleweka isiyo badilika mara kwa mara, anapaswa asiwe kama kasuku kwamba leo ataandika suala la mapenzi kesho ataandika suala la siasa, endapo kama mwandishi hatakuwa na falsafa inayoeleweka atayumbishwa na watu wengine hivyo kazi yake haitakuwa na msimamo. Mfano wa waandishi wenye falsafa inayoeleweka ni Wole Sonyika pamoja na Ngungi Wa Thiong'o.

Hivyo basi mwandishi huru ni yule anayeweza kutetea na kuisemea jamii yake kuhusu matatizo bila kikwazo, kwa hiyo ni vyema waandishi watambue kuwa uhuru wao unatokana na wao wenyewe jinsi watakavyowasilisha kazi zao kwa jamii endapo kama watafuata vigezo hivyo hakuna yeyote atakayeingilia kazi zao wala kuipinga.


Kielelezo 1.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kufafanua mambo yanayomfanya mwandishi wa fasihi kuwa huru katika kuitetea jamii yake.

Aidha, watahiniwa wachache (15.5%) walitoa hoja na maelezo yasiyokuwa na mifano na pia miongoni mwao walishindwa kutoa utangulizi mzuri na hitimisho zuri na hivyo kupata alama 7 hadi 11.5 ambazo ni alama za wastani.

Hata hivyo, asilimia ndogo sana (1.2%) ya watahiniwa waliofanya swali hili walishindwa kueleza mambo manne muhimu yanayoweza kumfanya mwandishi wa kazi ya fasihi kuwa huru kuandika ama kukosoa jambo lolote bila kikwazo na hivyo kupata alama 0. Watahiniwa hao walishindwa kueleza hoja kama vile ; msimamo na falsafa ya mwandishi na namna mwandishi anavyoweza kufanya ubunifu katika kuitawala lugha. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika mambo yanayohusu dhima ya kazi za fasihi kama vile *kuelimisha jamii, kuikomboa jamii na kuishauri jamii* badala ya kueleza masuala yanayohusu

uhuru wa mwandishi. Kielelezo 1.2 kinaonesha mtahiniwa aliyeandika hoja tofauti na matakwa ya swali.

**Kielelezo 1.2**



1. Uhuru wa mwandishi ni ule uhuru ambao anaweza kuandika kazi yake (zake) bila ya kuwe na matatizo yoyote katika jamii. Hivyo basi, mwandishi yeyote atakuwa kuwa huru pindi pale tu ataweza kufanya mambo yafuatayo;

Kuelimisha jamii, mwandishi wa kazi yoyote ya fasihi ataweza kuwa huru pale tu anapoelimisha jamii yake katika masuala mbalimbali. kwa mfano, masuala ya uchumi, kitamaduni, kisiasa na kijamii.

Kuikomboa jamii, mwandishi wa kazi ya fasihi ataweza kuwa huru pale tu anapoikomboa jamii katika fikra mbovu za unyonyaji na kugandamizwa. Hivyo utasababisha jamii husika/fulani kuwa na uhitaji zaidi ili iweze kutoka katika mifumo mbalimbali ya uovu,


Kuiburudisha jamii; mwandishi yeyote wa kazi ya fasihi ataweza kuwa huru anapoiburudisha jamii kwa kuandika kazi mbalimbali ambazo zinawangiambe wa kumfanya msomaji aweze kufurahi na kupenda kazi hiyo. Hivyo huweza kumfanya mwandishi huyo kupendeka kwa jamii fulani/husika.

Kuishauri jamii husika, mwandishi anakuwa/atakuwa huru endapo ataweza kuishauri jamii kuondokana na mambo mbalimbali.

Kielelezo 1.2 kinaonesha sampuli ya sehemu ya jibu la mtahiniwa aliyeandika dhima mbalimbali za fasihi badala ya kuandika mambo yanayompa uhuru mwandishi katika kuiandika kazi yake.

### 3.2.2 Swali la 2: Fasihi kwa Ujumla.

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi kwa Ujumla* na lililenga kupima majazi ya utambuzi ngazi ya uchambuzi. Swali lilikuwa na jumla ya alama 20 na lilimtaka mtahiniwa kutaja na kueleza mambo matano yanayofanya usanii wa kifasihi kuwa tofauti na usanii wa sanaa nyinginezo kama vile; uchongaji na ususi. Watahiniwa wengi (71.6%) kati ya waliofanya mtihani walijibu swali hili. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili na kufaulu kwao kiasilimia kumefafanuliwa vizuri katika Chati Na. 6 kwa kuonesha kufaulu kwa kiwango hafifu, kufaulu kwa kiwango cha wastani na kufaulu kwa kiwango kizuri.




**Chati Na. 6**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Asilimia 97.1 ya watahiniwa hao walipata alama 7 hadi 19.5. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kwani watahiniwa wengi (82.7%) walifanya vizuri na kupata alama 12 hadi 19.5. Baadhi ya watahiniwa hao waliopata alama za juu waliweza kutoa utangulizi mzuri, kutaja mambo matano yanayofanya usanii wa kifasihi kutofautiana na fasihi nyingine kama vile ; mpangilio mzuri wa matukio yaani muundo, uteuzi mzuri wa lugha, uumbaji wa wahusika na mandhari. Kielelezo 2.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri kwa kuonesha tofauti kama vile : *uwepo wa wahusika, lugha, mandhari na utendekaji* katika usanii wa kifasihi.


**Kielelezo 2.1**

Fasihi ni Sanaa inayotumia lugha ilikufikisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa, lakini Sanaa ni ufundi au umbo lililosanifiwa na kufinyangwa kwa ujuzi fulani ilikuleta mvuto katika kazi ya kifasihi kuna aina mbili za fasihi nazoni fasihi andishi na fasihi Simulizi, lakini Sanaa kunaaina nyingi mfano uchongaji, uchoraji, ususi, muziki, ufinyanzi na Sanaa zingine nyingi. Hivyo basi Usanii wa ~~fa~~ kifasihi ni zaidi ya usanii wa uchongaji au ususi kwa hoja zifuatazo fasihi na Sanaa zinatofautiana.

**Wahusika**, Usanii wa kifasihi huhusisha fanani na hadhira ambao huonana ana kwa ana, lakini usanii wa uchongaji au ususi huhusisha mtendaji tu (fanani) bila ya kuwepo kwa ~~fa~~ hadhira itakayo mpongeza au kupiga makofi wakati wa uchongaji au ususi.

Uwepo wa Lugha. Usanii wa kifasihi hutumia Lugha, kwani lugha ndiyo nyanja kuu katika Usanii wa kifasihi kwa sababu Lugha ndiyo ~~mal~~ inaelezea fasihi yenyewe kuwa fasihi ni Sanaa inayotumia Lugha kufikisha ujumbe wake, lakini usanii wa uchongaji au ususi wenyewe hautegemei lugha bali unategemea Vifaa kama vile panga ya kukatia magogo Shoka, tezo au Nyuzi za katani kusokota kamba bila ya kutumia Lugha yoyote.

Uwepo wa mandhari au (mazingira), fasihi huhitaji uwanja wa kutendea tukio, usanii wa kifasihi bila Mandhari huo siyo usanii wa kifasihi kwa Sababu fasihi kama fasihi hutawaliwa na Mandhari, Sehemu tukio la kisanaa linapotendeka lakini usanii wa uchongaji au ususi wenyewe hauhitaji mazingira maalumu kama fasihi.


Q. Utendekaji. katika usanii wa kifasihi dhana ya utendekaji ni muhimu kuonekana kwa sababu fanani na hadhira wanatenda matendo kwa hadharani pia fanani na hadhira huonesha dhana hii ya utendekaji kwa kutende matendo halisi katika uigizaji wao, lakini usanii wa uchongaji au ususi wenyewe hauna dhana ya utendekaji.

Usanii wa kifasihi wenyewe una sehemu kuu mbili ambazo ni fani na maudhui, katika usanii wa kifasihi fani na maudhui huonekana kutokana na mandhari, wahusika, lugha iliyotumika utendaji wa wahusika hii yote hubeba dhana ya fani na maudhui katika usanii wa kifasihi lakini katika Usanii wa uchongaji au ususi fani na maudhui haviwezi kujitambana moja kwa moja.

Kwa kuhitimisha fasihi na sanaa zina fanana na kutofautiana katika nyanja mbalimbali mfano Lugha, wahusika, utendekaji, ubunifu, mandhari, fani na maudhui.

Kielelezo 2.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kufafanua mambo yanayotofautisha usanii wa fasihi na usanii mwingine kama vile ususi na uchongaji.

Hata hivyo, watahiniwa wachache (14.4%) walishindwa kutoa utangulizi mzuri, mpangilio mzuri wa matukio yaani muundo katika kazi za kifasihi na hivyo kuwafanya kupata alama 7 hadi 11.5 ambazo ni alama za wastani.

Aidha, asilimia 2.9 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata alama chini ya 7 ambapo miongoni mwao asilimia 0.1 walipata alama 0. Baadhi ya watahiniwa hao walitoa hoja chache ambazo hazikuwa na ufafanuzi wa kutosha. Aidha, watahiniwa wengine waliandika hoja ambazo hazikuwa na uhusiano na kile kilichoulizwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika hoja kama vile; '*kuelimisha jamii*', *kukosoa* jamii, *kuakisi yaliyomo*

*kwenye jamii* ', vilevile aliandika *kutambulisha jamii fulani*, hoja ambazo hazikuwa sahihi. Kielelezo 2.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu kinyume na mahitaji ya swali.


**Kielelezo 2.2**

2. "Usanii wa kifasihi ni zaidi ya usanii
wa uchongaji au uvusi". Hoja zifuatazo zina-
~~thibith~~ thibitisha kauli hiyo ya kuwa fasihi
yaani usanii wa ~~ufasihi~~ ni mkubwa kuliko usanii
wa uchongaji au uvusi

Kuelimisha jamii, usanii wa kifasihi
ni zaidi ya usanii wa uchongaji au uvusi kwani
usanii wa fasihi huelimisha jamii kupitia kazi
tofauti za fasihi mfano mwaya, taarabu,
muziki na mashairi.

Vilevile usanii wa fasihi hukosoa jamii,
usanii wa fasihi hukosoa jamii kutokana na
mambo mbalimbali yanayofanyika katika jamii
yetu ambayo siyo mazuri. mfano, rushwa sana
sana kwa viongozi wetu, hivi hutumia kazi
mbalimbali za fasihi mfano. mashairi

Pia usanii wa fasihi hutambulisha
jamii kutokana na mambo ambayo yanafa-
nyika katika jamii hiyo, kupitia usanii wa fasihi
huwa inawezekana wa kutambulisha jamii na
kuweza kutofautisha jamii moja na nyingine ~~kuto~~-
kutokana na mambo yanayoendelea ~~y~~ au yanayofanyika
katika jamii hiyo.



Usani wa fasihi pia huakisi yaliyomo kwenye jamii, hii ni kupitia kazi mbalimbali za fasihi ambazo zinasaidia kuakisi kinachofanyika au kinachoendelea ndani ya jamii, ndio maana husemwa kuwa usanii wa fasihi ni zaidi ya usanii wa uchongaji au ususi.

Pia usanii wa fasihi vilevile huta-mbulisha tamaduni fulani, hii ni moja ya mambo ambayo yanafanya usanii wa kifasihi tofauti na usanii wa sanaa nyingine kwani kupitia usanii wa fasihi inawezesha kujua tamaduni ya jamii fulani mfano, mwaya ya "kuta nkwile" sanaa ya fasihi inatambulisha tamaduni ya wahindi.

Hivyo kutokana na mambo hayo ndio maana inasemwa kuwa usanii wa fasihi ni zaidi ya usanii wa uchongaji au ususi kwani usanii wa kifasihi kuwa na mambo mengi yanayo kuwa na matokeo chanya kwa jamii kwa mengi na maendeleo ya jamii.

Kielelezo 2.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeeleza dhima za fasihi badala ya kueleza mambo yanayofanya usanii wa kifasihi kuwa tofauti na usanii wa sanaa nyingine.

## 3.3 SEHEMU B: USHAIRI

### 3.3.1 Swali la 3: Uhakiki wa Ushairi

Swali lilihusu mada ya *Ushairi*, lililenga kupima tathmini na lilikuwa na jumla ya alama 20. Aidha, swali lilimtaka mtahiniwa kutetea usemi usemao kuwa ‘‘Washairi wengi ni jasiri katika kufichua maovu yaliyopo katika jamii ili kuziimarisha.’’

Swali lilijibiwa na watahiniwa wengi (94.5%) kati ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Miongoni mwa watahiniwa hao, asilimia 98.9 walipata alama 7 hadi 19.5. Kati ya hao, asilimia 87.9 walifanya vizuri na kupata alama 12 hadi 19.5. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kutokana na watahiniwa wengi waliopata alama za juu kwa, viwango tofauti kuweza kuonesha maovu mengi yaliyofichuliwa na washairi kama vile; *kupinga rushwa, ukoloni mamboleo, kukemea uongozi mbaya unyonyaji/unyanyasaji, usaliti na wizi* na *pia kuiasa jamii kuwa na maadili bora*. Kielelezo 3.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyetoa hoja sahihi na kuzifafanua ipasavyo kwa kila diwani.

**Kielelezo 3.1**

3. Washairi ni watumizi wa utanzu wa ushairi ambao hutumia ufundi mkubwo kujenga kazi zao ambazo huwasilishwa kwa beti na mistari. Maovu ni mambo yasiyokubalika katika jamii au yanayokiuka Miiko ya jamii. Lengo la washairi wengi ni kuibua Maovu yanayotendeka kwa ajili ya kufumbua macho wananchi ili waweze kuelewa na kutafuta mbinu za kuyatatua. Kwa kutumia kitabu cha Ushairi "FUNGATE YA UHURU" kilichoandikwa na Mohamed S. Khatibu kinathibitisha usemi huo wa washairi kama ifuatavyo;

Rushwa; Ni kitendo cha kupokea kitu cha thamani/pesa isiyo halali kwa lengo la kufanya kitu fulani. Katika diwani hii mwandishi amedhihirisha rushwa inayofanywa na viongozi wa Afrika kwa ajili ya kuuza haki katika Shairi la "Viongozi wa Afrika"

"Viongozi wa Afrika
wanaokula rushwa
haki ya mtu kununua"

Huu ni uovu uliopo katika ngazi ya uongozi ambayo ni halisi mpaka sasa.

Ukoloni Mamboleo; Ni mfumo mpya wa ukoloni ~~ambayo~~ ambao wakoloni waliopita wanaendelea kutunyonya kwa ufiche kisiasa, kiutamaduni na ~~kiuto~~

hata kiuchumi. Ukoloni mamboleo umeongeleshwa na Mshairi katika shairi la "Nguruwe" na pia shairi la "Afrika" linalosema,

"Bara la Amerika, Na Ulaya kadhalika
Kwamestaarabika
Kuinyonya Afrika
Nasi tukafukarika"

Shairi hili linafichua uwazi wa badhi ya ~~wa~~ mataifa yanayotunyonya na kutufanya tufukarike (maskini) kwa kupitia viongozi wetu.

Wizi: Ni kitendo cha kuchukua kitu/mali bila idhini ya mwenye nacho au kwa Magendo. Katika ushairi huu mshairi amefanikiwa kuibua wizi kama uovu uliokithiri jamii ya sasa katika nchi yetu (zetu za kiafrika). Mshairi ameonyesha haya katika shairi la "Paka Shume" na shairi la "Wizi" ambalo linasema,

"Wizi umo
kani sani
Msikitini
Wanyonywao ni waumini"

Mwandishi ameonyesha katika shairi hili la wizi uliyotapakaa kila nyanja ya maisha hadi katika nyumba za kuabudu.

Uongozi Mbaya: Huu ni uongozi usiojali matakwa ya wananchi, na pia uongozi uliojaa maovu, unaoshiriki kidna na wakoloni kuinyonya nchi. Mshairi

3 ameonyaonyesha haya katika shairi la "Tume salitiwa" na shairi la "Viongozi wa Afrika" kama linavyosema,

"Viongozi wa Afrika
Wanaokula mapesa
Wakaongeloa anasa"

Pia

"Viongozi wa Afrika
Wanaohongwa mapesa"

Mashairi haya yanathibitisha uongozi mbaya wa viongozi wetu kwa mambo wanayoyafanya. Pia katika shairi la ~~TUNGATE~~ "tungate" linadhihirisha uongozi huu mbaya ambao ~~kwa~~ bado upo katika kusherehekea miaka saba ya uhuru. Kwa kutumia kitabu cha "KIMBUNGA" kilichoandikwa na Haji Gora hoja ya maovu inadhihirishwa kama ifuatavyo;

Rushwa: Mwandishi ameonyesha Rushwa inavyoharibisha waafrika na jamii kwa ujumla. Mshairi anaonyesha Rushwa katika shairi la "Rushwa" kama linavyosema,

~~Rushwa kajenga~~

"Rushwa kajenga kambi, na kuondoka hataki
Mkaidi hashindiki, hapingiki mkaidi.
Tumzushieni wimbi, isiwe kutuhiliki
Tumchimbie handaki, Rushwa tukamzikeni"

Hapo mwandishi anaonyesha namna ambavyo rushwa imekomaa na pia anashauri jamii kupiga vita rushwa na kuizika.

3. Unyonyaji/Unyanyasaji: Ni kitendo cha kumtendea binadamu mwenzako kinyume na haki yake kwa sababu ya udhaifu wake. Mshairi ameonyesha unyonyaji katika shairi la "Wenye Vyao Watubana" kama linavyosema,

~~Wenye vyao watubana, watutubwa tuteteeni~~


"Wenye vyao watubana, Maskini twaumia,
La kuwafenyiza hatuna, hali zetu taabuni,
kwa sasa bei ya dona, kilo mia ishirini
Walakubwa tuteteni, wenye vyao watubana"

Katika shairi hili tunaona maskini wasio kuwa nacho wanavyoonewa na wenye navyo (Matabaka).

Usaliti: Ni ~~kitendo~~/hali ya kwenda kinyume na maazimio baina ya watu wengi au mtu na mtu. Katika shairi la "Kimbwangai" ambayo ni taswira ya Viongozi wasaliti mshairi ameonyesha namna viongozi wanavyowasaliti wananchi waliowaweka madarakani.

"Kimbwangai lipoona
~~Ni mtu kakamiliya~~
ni mtu, binadamu kakamiliya
akaanza kujivuna
akasahau ni nyani asilia"

Katika shairi hili kimbwangai alitumwa na nyani wenzake, ambayo ni taswira ya wananchi na viongozi waliko madarakani, lakini kimbwangai (kiongozi) aliwasaliti nyani (wananchi).





Kielelezo 3.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kufafanua vyema suala zima la kufichua maovu yaliyopo katika jamii ili kuziimarisha kwa kutoa mifano maridhawa.

Aidha, asilimia 11 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata alama 7 hadi 11.5 ambazo ni alama za wastani kwa sababu waliweza kutoa hoja za maovu yaliyopo katika jamii bila kuonesha mifano kutoka katika mashairi yanayodhihirisha maovu hayo yanayokemewa na wasanii kama ilivyohitajika katika swali.

Ijapokuwa watahiniwa wengi (87.9%) walijibu vizuri swali hili, asilimia ndogo sana (1.1%) ya watahiniwa hawakulijibu kwa usahihi na hivyo kupata alama 0 hadi 6.5. Miongoni mwa watahiniwa hao asilimia 0.1 walipata alama 0 kutokana na kutokuwa na maarifa ya kutosha katika dhana nzima ya ushairi, taratibu za uandishi na matumizi ya lugha sanifu kwani hawakuweza kutoa hoja zenye ufafanuzi toshelevu. Kielelezo 3.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa kufuata matakwa ya swali.

**Kielelezo 3.2**


3. Washairi wengi ni yasiri katika kufichua maovu yaliyopo katika jamii hii kuzumarisa kwa kutumia ~~Shair~~. Diwani ya "Chungu Tamu" iliyoandikwa na Theobald A. Mvungi pamoja na "Fungate ya Uhuru" iliyoandikwa na Mohamed S. Khatib

Kwa kuanza na "Chungu Tamu" maovu yafuatayo yame~~chu~~ onekana katika diwani hii

Uongozi ~~mp~~ mbaya; katika diwani hii msanii ameonesha jinsi gani viongozi hao wanajibika kwa kutumia shairi la ~~Viongozi wa A~~ "Wimbo wake hotuba" linalosema


"Cheo kiko mkononi
Agizo li mdomoni
Wimbo wake hotuba

Kielelezo 3.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyetumia kitabu kimoja tu cha ushairi na pia alishindwa kufafanua hoja yake moja aliyoitoa.

### 3.3.2 Swali la 4: Uhakiki wa Ushairi

Swali lilihusu *Ushairi* na lilimtaka mtahiniwa kuonesha masuluhisho manne yaliyotolewa na washairi ili kukabiliana na changamoto zinazohusiana na kukosekana kwa uzalendo katika jamii. Swali lilikuwa na jumla ya alama 20 na lililenga kupima tathmini.

Swali lilijibiwa na watahiniwa wachache sana (5%) kati ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili na kufaulu kwao kiasilimia kumewasilishwa vizuri katika Chati Na.7 kwa kuonesha kufaulu kwa kiwango hafifu, kufaulu kwa kiwango cha wastani na kufaulu kwa kiwango kizuri.




**Chati Na. 7**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kwani asilimia 98.5 ya waliolijibu walipata alama 7 hadi 19 ambapo asilimia 89.2 walifanya vizuri na kupata alama 12 hadi 19. Baadhi ya watahiniwa hao waliweza kuonesha masuluhisho machache lakini yaliyokuwa na ufafanuzi uliojitosheleza. Aidha, idadi kubwa ya watahiniwa waliofanya vizuri waliweza kuandika masuluhisho manne yaliyotolewa na washairi ili kukabiliana na changamoto zinazohusiana na ukosefu wa uzalendo katika jamii. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitumia diwani ya *Kimbunga* na *Chungu Tamu*. Katika diwani ya *Kimbunga* alitoa masuluhisho kama vile; *kupiga vita uongozi mbaya na rushwa* kwa kurejea shairi la ‘Kimbunga’ na ‘Madanganyo’. Kwa upande wa diwani ya *Chungu Tamu* alitoa masuluhisho kama vile; *kupiga vita matabaka* kwa kurejea shairi la ‘Chatu na Kuku’, *kufanya kazi kwa bidii* kwa kurejea shairi la ‘Daktari Askari’, *kupiga vita uongozi mbaya* kwa kurejea shairi la ‘Tishio la Binadamu’ na ‘Kademokrasia Kametoweka’, *kuwa na mapenzi ya kweli na nchi* kwa kurejea shairi la ‘Daktari Askari’. Vilevile mtahiniwa aliweza kutoa utangulizi na hitimisho linaloendana na swali kama Kielelezo 4.1 kinavyoonesha.

**Kielelezo 4.1**

4 Uzalendo ni hali ya mtu kuip
enda, kuitumikia na kuilinda nchi
yake. Ukosefu wa uzalendo limekuwa
tatizo katika jamii za kiafrika, na ndilo
lililowashughulisha washairi mbalimba
li. Hili limeonyeshwa na kutolewa sulu
hisho katika diwani mbili ambazo ni
KIMBUNGA kilichoandikwa na HAJI GORA
HAJI na diwani ya CHUNGU TAMU ili
yoandikwa na THEOBALD MVUNGI. Hiv
a washairi wameweza kutoa masuluhisho
pia ya suala la kukosa uzalendo.

Kwa kuanza na kitabu cha
KIMBUNGA mshairi ameonyesha sulu
hisho la kupiga vita uongozi mbaya.
Jamii za kiafrika zimekumbwa na tatizo
la uongozi mbaya, hili limeonyeshwa kati
ka shairi la "Kimbunga" ukurasa wa 1
kutokana na uongozi mbaya mwandishi
anaona ni vyema mapinduzi yafanyike
ili kuleta uongozi bora, pia katika shairi
la madanganyo ukurasa wa 6 mshairi
anaonyesha wananchi wanavyodanganywa
na viongozi wao hivyo lazima kupiga vita
uongozi mbaya ili kuleta uzalendo
Kupiga vita rushwa, Uzalendo
umepotea kutokana na suala la rushw
a, hili limeonyeshwa katika shairi la
Rushwa ukurasa wa 12 na madhara
yake kwa jamii, Hivyo anawataka wana
jamii kupiga vita kwa nguvu zote suala
la rushwa ili kuleta uzalendo katika nchi.

4. Kupiga vita ukoloni mamboleo
Suala hili limemshughulisha mwandishi kwa kulionyesha katika shairi la Chuwi ukurasa wa 42. Jamii nyingi za Afrika zimeathiriwa kiuchumi, kitamaduni na kisiasa kutokana na suala la ukoloni mamboleo, hivyo mshairi anasisitiza wanajamii wapige vita ukoloni mamboleo ili kujenga uzalendo katika nchi zetu.

Kufanya kazi kwa bidii na kujituma. Ili wanajamii waweze kujenga jamii yao na kujihudumia, mshairi amesisitiza bidii katika kazi kwenye shairi la kazi ukurasa wa 17-18, hivyo anawasisitiza wanajamii kuachana na uzembe ili kujenga uzalendo wa kuihudumia jamii yote.

Pia katika diwani ya CHUNGU TAMU mshairi ameonyesha suala la kupiga vita matabaka, mshairi ameliomyesha hili katika shairi la chatu na kuku ukurasa wa 2 akionyesha tabaka kati ya wanyonyaji na wanyonywaji, watawala na watawaliwa, pia katika shairi la Thomas na Dotto mshairi ameonyesha tabaka kati ya mzungu na mwafrika japo Thomas na Dotto waliondoa utabaka. Hivyo lazima matabaka yapingwe ndani ya jamii.

Kufanya kazi kwa bidii.
Mshairi amelionyesha hili katika shairi la ~~Kazi~~ Daktari Askari ukurasa wa 11 ambapo madaktari, manesi na wanajeshi

walipambana ili kuikomboa nchi yao na
4, jamii yao, Hivyo kufanya kazi kwa bidii
ni njia ya kujenga uzalendo katika jamii.
Kupinga uongozi mbaya.
Msanii ameonyesha uongozi mbaya kama
kikwazo cha uzalendo, hili limeonekana
katika shairi la Tishio la binadamu uku
rasa wa 2 kwa nchi zenye nguvu kugan
damiza nchi za Afrika, shairi la kademokrasi
katoweka, mshairi anaonyesha utengenezwa
ji wa silaha za vita, pia katika shairi la
wenye vyao watubana, ameonyesha jinsi
watawaliwa wananyanyaswa. Hivyo kupin
ga vita uongozi mbaya ni suluhisho la
kuleta uzalendo.
Kuwa na mapenzi ya kweli kwa
nchi. Mfano katika shairi la Daktari Askari
~~mwana~~ ukurasa wa 11 mwandishi ameonye
sha jinsi ambavyo watu mbalimbali waliji
toa muhanga katika kuikomboa nchi yao mfa
no wanajeshi, madaktari na manesi hivyo
hawa walikuwa na mapenzi ya kweli ndio
maana waliikomboa. Hivyo wanajamii wawe
na mapenzi ya kweli ili kuleta uzalendo.
Hata hivyo, uzalendo ni utama
duni wa jamii ni vyema wanajamii wa
fundishwa, watoto mashuleni na vyuo
vikuu ili kupandikiza moyo wa uzalen
do kwa nchi yao, wote wasiokuwa na
uzalendo wakibainika wafungwe ili
kupata adabu na mwenendo mwema
wa jamii.

Kielelezo 4.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri kwa kuonesha masuluhisho yanayotolewa na washairi katika kukabiliana na kukosekana kwa uzalendo katika jamii.

Hata hivyo, idadi ndogo (9.3%) ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 7 hadi 11.5 ambazo ni alama za wastani kutokana na kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu majina ya vitabu husika vya ushairi. Baadhi ya watahiniwa hao walichanganya majina ya shairi na wengine walishindwa kuonesha wazi masuluhisho yaliyooneshwa na washairi ili kukabiliana na changamoto za ukosefu wa uzalendo katika jamii.

Aidha, watahiniwa wachache sana (1.5%) kati ya waliofanya swali hili walishindwa kulijibu kwa usahihi na hivyo kupata alama 0 hadi 6.5 ambapo miongoni mwao asilimia 0.2 walipata alama 0. Baadhi ya watahiniwa hao waliandika hoja ambazo ni tofauti na mahitaji ya swali. Watahiniwa wengine walichanganya vitabu husika hasa katika kurejea mashairi ya diwani hizo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza baadhi ya dhamira zinazopatikana katika diwani ya *Chungu Tamu* badala ya kueleza masuluhisho yaliyotolewa na msanii katika kukabiliana na changamoto zinazohusiana na kukosekana kwa uzalendo katika jamii. Aidha, mtahiniwa huyo alitumia riwaya ya *Kufikirika* ambayo haina uhusiano na ushairi. Kielelezo 4.2 ni mfano dhahiri wa mtahiniwa wa aina hiyo.

**Kielelezo 4.2**

SEHEMU B:

4. Suala la uzalendo katika Diwani ya Chungu Tamu msanii ameonesha kwa kutumia dhamira mbalimbali.

Hoja ya kwanza dhamira uzalilishaji wa mwanamke msanii amechora namna ambavyo mwanamke anazalilishwa kwa kuwekwa utawani kama samaki wa kufugwa.

Hoja ya pili msanii Chungu Tamu amechora jamii kwa dhamira ya utumwa, msanii ameonesha dhamira yake hii kwa kumtumia mwanamke wa Kitanzania

Hoja ya tatu msanii amechora jamii kwa dhamira ya kujitoa muhanga kwa ajili ya ukombozi wa mtu mmoja mmoja lakini pia kwa Taifa zima.

Hoja ya nne

msanii amechora yeye mwenyewe kuwa ni mwana mapinduzi halisi ame fikisha mawazo yake kwa jamii juu ya kujikomboa.

Katika kitabu cha Kufikirika na Shaaban Robert. Uzalendo ni dhamira kuu katika kibu hiki

Hoja ya kwanza mfalme na malikia walikuwa ni wazalendo katika nchi yao ya kufikirika hata kufa, hata mtoto wa mfalme alipo ugua.

Hoja ya pili yule mwanasheria Kamara amesadifu uzalendo alikubali kutetea haki za watu wa kusadikika hata kufa.


Hoja ya tatu wajumbe kutoka pande kuu nne za dunia walikubali kupambana hata walipopelekwa ngerezani kwa ajili ya uzalendo.

Kielelezo 4.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeeleza dhamira badala ya masuluhisho ya kukabili ukosefu wa uzalendo katika jamii. Vilevile mtahiniwa huyo alitumia diwani ya *Chungu Tamu* pamoja na riwaya ya *Kufikirika* badala ya kutumia vitabu vya ushairi pekee.

## 3.4 SEHEMU C: RIWAYA

### 3.4.1 Swali la 5: Uhakiki wa Riwaya

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Andishi* hasa kuhusu vitabu teule vya Riwaya na lililenga kupima uchambuzi. Swali lilimtaka mtahiniwa afafanue faida za kazi za fasihi andishi kwa jamii ya Tanzania kwa nyakati zote na lilikuwa na jumla ya alama 20. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili na kufaulu kwao kiasilimia kumefafanuliwa vizuri katika Chati Na. 8 kwa kuonesha kufaulu kwa kiwango hafifu, kufaulu kwa kiwango cha wastani na kufaulu kwa kiwango kizuri.





**Chati Na. 8** : Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Swali lilijibiwa na asilimia 63.7 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Asilimia 99.1 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 7 hadi 19.5. Miongoni mwa watahiniwa hao, asilimia 92.2 walipata alama 12 hadi 19.5. Baadhi ya watahiniwa hao waliofanya vizuri waliweza kufafanua faida mbalimbali zinazoweza kupatikana katika riwaya mbili walizosoma kwa jamii ya Tanzania. Faida hizo ni kama vile; kuelimisha jamii na kutoa ufumbuzi wa matatizo mbalimbali ambayo jamii imeweza kufaidika na kubadilika. Watahiniwa wengine waliopata alama za juu waliweza kufafanua faida kama vile umuhimu wa

uwajibikaji, kudumisha na kuyaenzi mapenzi ya kweli, umuhimu wa elimu, kufanya kazi kwa bidii na kuepuka tamaa ya fedha. Kielelezo 5.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

**Kielelezo 5.1**


5. Mwandishi ni mtu anaechukua muda wake mwingi ili kuweza kuongea na jamii yake kwa maandishi. Wasanii wa kazi za fasihi, hufanya kazi zenye tija kubwa kwa jamii ya Tanzania nyati 2016. Hii ni kweli kwani kila kazi ya fasihi inafaida kwa mfano kufundisha, kuburudisha, kukosoa jamii na mengineyo, na pia huonesha yaliyopo katika jamii. Kwa kutumia "Mfadhili" ya "Hussein Tuwa" na "Vuta N'kuvute" ya "Shafi Adam Shafi", wameweza kutumia maudhui kuonesha/kufanya kazi yao yenye tija kubwa kwa jamii kama ifuatavyo kuanzia na "Mfadhili" ya "Hussein Tuwa" ameonesha ;

Suala zima la mapenzi na ndoa. Mwandishi ameliomesha suala hili katika sura mbili, mapenzi ya kweli na mapenzi ya uongo. Mapenzi ya ukweli yameoneshwa kama ni chanzo cha furaha, amani na ufanisi katika kazi kwa mfano Gaddi Bullah walivyo anza uhusiano wa kimapenzi na Dania Theobald, wote wawili walitu-a na furaha na waliweza kufanya kazi. Pia, mapenzi ya uwongo yamechorwa kama ni kikwazo cha maendeleo kwani kinapunguza ufanisi wa kazi kwa mfano pale Gaddi Bullah alipoachishwa na Mkewe Nyambuja alizorota kazini na hatimaye atashushwa cheo na kuhamishwa. Hivyo, msanii amehimiza kwa kamwe hakuna uwiano kati ya mapenzi na mambo ya kazi.

Usaliti. Msanii ameweza kuonesha suala la usaliti jinsi linavyokuwa linaendelea katika-

5 - jamii. Usaliti upo wa aina nyingi kwa mfano katika mapenzi, undugu, kazini, serikali kwa sasa na kadhalika ila mwandishi huyu ameongelea sana athari zake katika kazi (usaliti wa mapenzi katika kazi). Kwa mfano Gaddi Bullah alivyosalitiwa na Nyambuye ~~alidh~~ alivuliwa na cheo na kuhamishwa na alipo salitiwa na Dania mpaka akauawa na kuhama mji. Hivyo, ameonesha kuwa usaliti una athari mbaya sana.

Chanzo cha chuki. Mwandishi ameweza kuonesha vyanzo mbalimbali vya watu kupat-a hatua ya kuchukiana katika jamii. Hii imeoneshwa na Bi. Hanuna ambae aliwachukia sana ndugu, jamaa na marafiki wa Dania Theobald baada ya kumsaliti ndugu wake Gaddi Bullah na kumfanyia kitendo cha kuonewa Bi. Hanuna. Hivyo ikasababisha chuki dhidi yao.

Suala zima la uonevu. Pia, mwandishi ameonesha jinsi watu wanavyoendelea kuonewa katika jamii tena hasa kwa wale watu wa tabaka la chini. Kwa mfano pale Bi. Hanuna anapomwambia Nunu; "Mliniweka jela bila makosa". Hii inaonesha kuwa Bi. Hanuna alifungwa gerezani bila kosa lolote ila tu kwa sababu hana uwezo wa kufanya lolote na ndio maana akakuza chuki dhidi ya ndugu, jamii na marafiki wa Dania. Hivyo, ameonesha kuwa uonevu ni chanzo cha chuki.

Pia, katika riwaya ya "Vuta N'kuvute" ya "Shafi A. Shafi" ameonesha yafuatayo;

Athari za matabaka. Mwandishi ameonesha

5 - jinsi matabaka yanavyoendelea kukua katika jamii na kuonesha athari zake kwa wanajamii kuwa ni ukosefu wa maendeleo katika jamii. Hii inaoneshwa pale ndani ya Unguja jinsi ilivyo-kuwa na matabaka ya waarabu na waafrika, walio nacho na wasiokuwa nacho na mpaka kuna mahali tofauti baina ya wanajamii, sehemu za masikini na sehemu za matajiri. Hivyo, ameonesha kuwa matabaka ni kikwazo la maendeleo.

Ukoloni mamboleo. Hii ni hali ya nchi kuwa chini ya mamlaka ya nchi nyingine. Mwandishi ameonesha jinsi jamii yake inavyo kumbwa na tatizo hilo na kuwazindua wanajamii wenzake dhidi ya athari za ukoloni mamboleo. Hii inaoneshwa pale wazungu wanapopewa nafasi katika jamii kwa mfano Inspecta Wright na anawaweka watu wake kwa ajili ya kukoloni na athari zake ni kudidimia kwa maendeleo katika jamii.

Ujenzi wa jamii mpya. Mwandishi ametilia mkazo katika suala zima la ujenzi wa jamii. Jamii mpya itajengwa endapo kutatokea na mabadiliko hasa kisiasa na kiuchumi kwa mfano upigaji wa vita suala zima la unyonyaji. Ujenzi wa jamii mpya unaonesha na Denge na rafiki zake jinsi walivyokua wanajitahidi kupambana na wakoloni na kuwazindua watu macho juu ya suala hilo japo mwandishi hakuonesha hatima ~~yato~~ yao.

Suala zima la mapenzi na ndoa. Msanii ameonesha uwepo wa ndoa za mitala na mapenzi ya dhati pamoja na ya uwongo. Hii inaone-

5 -shwa na Yasmin ambae mara ya kwanza alila-
-zimishwa kuolewa na Mzee Razah wa miaka
50 na kuamua kumkimbia na pia ameonyeshwa
kuwa na mapenzi ya dhati kwa Bukheti na
Bukheti kwa Yasmin na pia ameonyeshwa kama
msaliti alipoamua kuachana na Denge bila kosa.
Hivyo, msanii ameshauri kuwa mapenzi na ndoa
ni baina ya watu wawili hivyo wajiamulie
na waachwe huru.

Hivyo, wasanii wa kazi za fasihi
hufanya kazi zenye tija kubwa kwa jamii ya
Tanzania nyakati zote kwani huonesha mambo
yote yanaendelea katika jamii na kuwapa ujumbe
jinsi ya kuyaepuka kama mabaya na kuyaendelez-
-a kama mazuri kwa kutumia mchakato
mzima wa maudhui.

Kielelezo 5.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeandika hoja zilizofafanuliwa vizuri na hitimisho linaloendana na swali.

Aidha, asilimia 6.9 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata alama 7 hadi 11.5 ambazo ni alama za wastani kwa sababu baadhi yao walishindwa kufafanua hoja walizozitoa kwa kinagaubaga. Watahiniwa wengine walitoa maelezo ambayo hayakujitosheleza kwani walishindwa kuonesha jinsi wasanii walivyoweza kuelimisha jamii na kutoa ufumbuzi wa matatizo ili jamii iweze kufaidika na kupata maendeleo.

Hata hivyo, asilimia ndogo sana (0.9%) ya watahiniwa waliofanya swali hili walishindwa kulijibu kwa usahihi na hivyo kupata alama 0 hadi 6.5. Miongoni mwao, watahiniwa wachache sana walishindwa kuandika utangulizi unaoendana na swali, kufafanua faida mbalimbali zinazoweza kupatikana katika riwaya mbili. Watahiniwa wengine walishindwa hata kutaja majina ya riwaya walizozitumia kutoa hoja zao hivyo kupata alama 0. Kielelezo 5.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa ambaye hakuweza kujibu swali hili ipasavyo.

**Kielelezo 5.2**

5. jamii nyingi hapa nchini Tanzania ~~zimefa~~-
zimekuwa na umoja na mshikano ili kuwe-
za kujenga jamii nzuri na maendeleo katika
riwaya hii, mwandishi anaeleza ~~kuwa~~/anaonye-
sha baadhi ya wahusika ambao waliungana na
kushirikiana katika kuleta maendeleo katika jamii.
mfano Yasmini, Denge na Mwajuma waliweza
kuungana na kuleta mabadiliko katika jamii.
Hitimisho, waandishi wa kazi za
fasihi wameweza kusaidia jamii nyingi
za Tanzania katika kuleta maendeleo ~~ya~~ na
kufanya mapinduzi kutokana na kazi zao
zimeweza kutoa ujumbe na kuelimisha jamii.

Kielelezo 5.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kikamilifu hasa katika kufafanua kwa kurejea katika vitabu teule vya riwaya.


### 3.4.2 Swali la 6: Uhakiki wa Riwaya

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Andishi* hasa kuhusu vitabu teule vya Riwaya na lililenga kupima majazi ya utambuzi ngazi ya uchambuzi. Swali lilikuwa na jumla ya alama 20 na lilimtaka mtahiniwa kuthibitisha jinsi mienendo ya wahusika wakuu ilivyofanikisha kuibua dhamira za waandishi katika riwaya mbili.

Swali lilijibiwa na watahiniwa wachache (36.1%) kati ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Miongoni mwa watahiniwa hao, asilimia 80.6 walilijibu vizuri kwani baadhi yao waliweza kuibua mienendo mbalimbali ya wahusika wakuu katika vitabu teule vya *Vuta Nkuvute* na *Usiku Utakapokwisha* na kupata alama 12 hadi 19. Baadhi ya mienendo hiyo iliibuliwa na wahusika wakuu Yasmin, Denge, Gonza na Chioko. Aidha, watahiniwa wengine waliopata alama za juu waliweza kuibua dhamira mbalimbali kama vile : *Usaliti, Ujasiri wa Mwanamke*

*katika kupinga mila potofu hasa kuhusu ndoa za utotoni, kupiga vita rushwa na wahujumu uchumi, dhuluma iliyokithiri katika jamii na matatizo ya usafiri yanavyokuwa kikwazo kikubwa katika jamii* pamoja na *kutetea utawala bora*. Kielelezo 6.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu swali hili kwa usahihi.

**Kielelezo 6.1**



6. Fasihi ni tanzu ya sanaa
inayotumia lugha kufundi zaidi ili
kufikisha ujumbe wake kwa hadhira
iliyo kusudiwa. Kazi ya fasihi inaundwa
na wahusika. Wahusika ni viumbe
ambao msanii anawatumia ili kuibua
dhamira mbalimbali katika kazi yake
ya fasihi. Kwa kuangalia riwaya ya
VUTA N'KUVUTE iliyoandikwa na
Shafi Adam Shafi msanii amemtumia
mhusika mkuu Yasmini kuibua dhamira.
Pia riwaya ya USIKU UTAKAPOKWISHA
msanii amewatumia wahusika wakuu
Gonza na Chioko kuibua dhamira
Kwa kuanza na mhusika mkuu
Yasmini katika riwaya ya VUTA N'KUVUTE
msanii ameibua dhamira zifuatazo:-
Usaliti, msanii amemtumia
Yasmini kuibua dhamira hii pale ambapo
Yasmini alimsaliti Koplo Matata na
kumweleza Denge siri aliyopewa. Hii
inaonekana ukurasa wa 154 anaposema
"Alimkabidhi Denge yale makaratasi" Koplo
Matata kanambia niyalete kwako
lakini wewe usijue kama nimeyaleta"
Huu ni usaliti, muuni kwani ulilenga
kuondoa ukandamizaji uliokuwa unafanya
na serikali ya kikoloni hivyo unapaswa
kuigwa katika jamii
Suala la ndoa, mwandishi
amemtumia Yasmini kuibua dhamira
ya ndoa za utotoni na ndoa za

6 kulazimishwa. Ndoa za utotoni msanii ameziomyesha ukurasa wa kwanza anaposema
"Mara tu baada ya kuvunja ungo
Yasmini aliozwa mume"
Hapa msanii anaonyesha kuwa ndoa hii ilikuwa ni ya umri mdogo na ndio maana haikudumu na kuvunjika. Jamii za sasa bado zinandoa za utotoni hivyo watu wanapaswa kubadilika na kuachana na mila hizi

Suala la mapenzi, msanii amemuonyesha Yasmini kama mwenye mapenzi ya dhati kwa Denge pale anaposema Denge kumwambia Yasmini
"Yasmini rafiki unanipenda na mimi nakupenda vilevile."
Hapa msanii anaonyesha upendo wa dhati kati ya Yasmini na Denge. Kwa jamii ya sasa inapaswa kuwa na mapenzi ya dhati ili kuepusha migogoro katika jamii

Wivu, msanii amemtumia Yasmini kama mtu ambaye anaonewa sana wivu na mume wake Shihab kwa sababu ya uzuri wake. Msanii anasema ukurasa wa 211
"Alikuwa hendi hamdi yumo ndani kama kizuka kwa sababu ya wivu aliokuwa nao Shihab"
Hapa msanii anaonyesha kuwa wivu

6 haufai katika jamii kwani unamnyima mtu haki zake za msingi, hivyo ni vizuri kwa jamii kupambana na uovu
Pia katika riwaya ya USIKU UTAKAPOKWISHA msanii amewatumia wahusika, wakuu Gonza na Chioko kuibua dhamira zifuatazo
Rushwa, msanii amemtumia Chioko kuibua dhamira ya Rushwa na pia Gonza kuibua rushwa pale Gonza anaposema katika ukurasa wa 81
"Mwambie shemeji ahonge bwana kama hana pesa kama sisi anaweza kutumia njia nyingine"
Hapa msanii anamchora Gonza kama mtu anayeshinikiza kumimiza rushwa. Rushwa haifai na inapaswa kupingwa katika jamii.
Dhuluma, msanii amemtumia Gonza kuibua dhamira ya dhuluma pale Gonza anaposema ukurasa wa 74
"Sikiliza wewe Chioko, unawaona wale watu wenye mifedha hapa mjini? Wengi wao wamedhulumu. Walishikwa? Hawakushikwa"
Hapa Gonza anaonyesha kuwa katika jamii kuna watu wana mifedha lakini wamezipata kwa dhuluma hivyo ni vizuri kwa jamii kusimama na kupinga dhuluma ya aina yoyote ile



6 Suala la mapenzi, msanii anamtumia Chioko kuibua suala la mapenzi kupitia kwa mpenzi wake Nelli pale anaposema
"Nelli ni waridi la moyo wangu mchanga"
Hapa msanii anaonyesha kuwa Chioko ana mapenzi ya dhati kwa Nelli. Mapenzi haya yanapaswa kuigwa katika jamii kwa sababu yanachochea maendeleo
Tatizo la usafiri, msanii anamuonyesha Gonza katika kituo cha mabasi ili kuibua dhamira ya tatizo la usafiri pale anaposema ukurasa wa 7,
"Walifika kituoni hapa, walikuta umma wa watu utadhani kulikuwa na sherehe ya kumtoa mwari na ambaye leo hii amefunga ndoa"
Hapa msanii anaonyesha kuwa katika jamii bado kuna tatizo la usafiri hivyo ni vema kwa serikali kuwekeza katika kuboresha vyombo na njia za usafirishaji
Waandishi Shafi Adam Shafi na Mbunda Msokile wamefanikiwa sana kuwaunda wahusika wao wakuu lakini pia waandishi hawa wamefanikiwa sana katika matumizi ya lugha kwa kutumia misemo, nahau, methali, tamathali za semi kama Tashibiha na upenzi wa Taswira.

Kielelezo 6.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kufafanua mienendo ya wahusika wakuu ilivyofanikisha kuibua dhamira mbalimbali katika riwaya teule.

Aidha, asilimia ndogo sana (17.2%) ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 7 hadi 11.5 ambazo ni alama za wastani. Baadhi yao walitoa hoja ambazo hazikujitosheleza. Kutokana na kushindwa kutumia lugha sanifu, kuzingatia taratibu za uandishi na hasa matumizi ya tahajia. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa waliandika majina ya wahusika kwa herufi ndogo na pia kutumia wahusika wadogo badala ya wahusika wakuu katika kujenga hoja zao. Kielelezo 6.2 ni mfano wa jibu la mtahiniwa ambaye alitumia riwaya ya *Mfadhili* na *Vuta N'kuvute* na kujadili wahusika wengi (wadogo) walivyoibua dhamira mbalimbali katika riwaya hizo badala ya kujadili wahusika wakuu pekee kama swali lilivyohitaji.

**Kielelezo 6.2**

SEHEMU C

6 Kwa Kutumia Kitabu cha Mfadhili
kicho andikwa na Hussein Tuwa na
Kitabu cha Vuta n'Kuvute kicho
andikwa na Shafi Adam Shafi -
Nashibitisha kauli hiyo kama ilivyo
Kwanza, katika kitabu cha
Mfadhili Muhusika Jerry amesa
babisha kuibuka kwa dhamira ya
Usaliti, baada ya kumtoroka Dania
kwenda Marekani wakati alimuahidi
atakuepo siku ya kufunga ndoa.
Pili, Chuki, dhamira ya Chuki
imeibuliwa na Dania wakati alipo
mchongea Gaddi ili afukuzwe kazi
dhamira hiyo ipo katika kitabu cha
Mfadhili.
Tatu, Upendo. dhamira hii
ya upendo imeibuliwa na daktari
Virani alipo msaidia rafiki yake
Gaddi alipo kuwa ana umwa na -

ugonjwa, shinikizo la moyo
Nne, Dharau. Dhamira ya dharau nayo inaibuliwa na mhusika - Nyambuja ambaye ni mke wa - Baddi Kitendo cha mke wa Baddi Nyambuja kufanya - mapenzi nje ya ndoa na rafiki - yake Baddi au kuondoka bila kumuaga ni moja ya dharau.
Tano, Ukombozi. Dhamira hii ya ukombozi inaibuliwa na mhusika Yasmini katika kitabu cha Vufa n'Kuvute. Yasmini alimkataa - Mzee Raza kumuoa kwani alikuwa mzee sawa na baba yake wa kumzaa.
Sita, Mapenzi ya pesa. Hii - imejitokeza katik kitabu cha - Vufa n'Kuvute baada ya - Mwajuma kumshauri Yasmini aachane na Denge kwa sababu - Denge hana pesa.
Saba, Ujasiri. Dhamira ya ujasiri - nayo inaibuliwa na Yasmini katika kitabu cha Vufa n'Kuvute Yasmini kitendo cha kutoroka kwa mume - wake na kuja kuishi kwa Mwajuma alionesha ujasiri mkubwa kama mtoto wa kike
Nane, Uwelewa. Kwa mara - nyingine Yasmini anaibua dhara ya uwelewa hii ni kutokana na -

Kujielewa ana nafasi gani katika maamuzi yomayo husi maisha yake. Tumeona katika kitabu cha Vuta-n' Kuvute Yasmini anejieleza bila woga kwa hayuko tayari kuolewa na Mzee Raza.

Mienendo ya wahusika ndio inayo ibua dhamira kama tulivyo ona katika vitabu vyote viwili; Vuta n' Kuvute na Mfadhili.

Kielelezo 6.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye alishindwa kuonesha tabia na mienendo ya wahusika wakuu inavyoibua dhamira mbalimbali, hivyo kupata alama za wastani.

Hata hivyo, watahiniwa wachache sana (2.2%) ndio walioshindwa kujibu vizuri swali hili na hivyo kupata alama chini ya 7. Miongoni mwa watahiniwa hao, waliopata alama za chini ya wastani walishindwa kithibitisha jinsi mienendo ya wahusika wakuu ilivyofanikisha kuibua dhamira za waandishi. Aidha, uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa hao hawakufuata matakwa ya swali kwani walijikita kueleza mienendo ya wahusika wadogo badala ya wahusika wakuu kama swali lilivyoelekeza.

## 3.5 SEHEMU D: TAMTHILIYA

### 3.5.1 Swali la 7: Uhakiki wa Tamthiliya

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Andishi*, lilihusu vitabu teule vya Tamthiliya na lililenga kupima uchambuzi. Swali liliwataka watahiniwa kufafanua mbinu tano kwa kila tamthiliya zilizopendekezwa na waandishi wa tamthiliya mbili kama nyenzo ya kujenga jamii mpya. Swali lilikuwa na jumla ya alama 20.

Asilimia 87 ya watahiniwa waliofanya swali hili walilijibu vizuri na kupata alama 12 hadi 19. Watahiniwa hao kwa

viwango tofauti waliweza kufafanua vizuri mbinu mbalimbali kama vile ; *umoja na mshikamano, kupiga vita uongozi mbaya, matabaka, dhuluma, unyanyasaji, umaskini* na *rushwa, umuhimu wa elimu* na *kuzingatia maadili ya jamii* kama mbinu zilizopendekezwa na wasanii katika kujenga jamii mpya. Kielelezo 7.1 kinaonesha mtahiniwa aliyeweza kujibu vizuri swali hili.

**Kielelezo 7.1**

7. Fasihi ni kazi ya sanaa inayotumia lugha ili kufikisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa. Waandishi wa kazi za fasihi ni watu wanaotumia muda wao katika kuandikia jamii juu ya mambo mbalimbali. Ujenzi wa jamii mpya ni hali ya kujenga jamii iliyoendelevu na kupambana na mambo yote yanayokwamisha maendeleo. Waandishi wa kazi za fasihi hulenga katika kuumba upya jamii zao kwa kutoa mbinu mbalimbali ili tu kuweza kujenga jamii iliyo mpya. Kwa kutumia tamthiliya mbili yaani "Nguzo Mama" chake Penina Muhando na "Kivuli Kinaishi" cha Said Mohamed waandishi hawa wameonyesha na kupendekeza mbinu mbalimbali zifuatazo ili kuweza kujenga jamii mpya. Kwa kuanza na kitabu cha "Nguzo Mama" mwandishi anapendekeza mbinu zifuatazo;

Umuhimu wa umoja na mshikamano; mwandishi anaona kuwa endapo kutakuwa na umoja na mshikamano miongoni mwa watu wa jamii fulani basi hii husaidia katika kuleta jamii mpya na yenye maendeleo. Kina mama wa kijiji cha Patata wanaamua kujiinua kiuchumi na kuw kujiendeleza kwa kufanya shughuli za ufumaji, upikaji wa pombe na kupika chakula. Katika kunyanyua kwa nguzo mama wanakosa umoja na mshikamano ili tu kuinua nguzo mama jambo linalopelekea nguzo kutoinuka. Kila mtu anategea na kwenda kufanya mambo yake na kuacha kuinua nguzo mama kama mwandishi anavyosema;

7. "...Sasa wewe Bi. Moja unaenda wapi?
7. Bi. Moja: Naenda bwana meli hii inipite..."

Kina mama hawa hawana umoja na mshikamano na pia hawakutaka kuwashirikisha wanaume kama mwandishi asemavyo;

"Bi. Nane: Tuwashilikishe na wanaume pia nguzo mama ina faida kwa wote...."

Lakini kina mama hawataki kuwashirikisha watu wengine jambo lililopelekea nguzo mama kutoinuka. Hivyo msanii anapendekeza kuwa ili kuweza kujenga jamii mpya lazima kuwepo na umoja na mshikamano baina ya watu.

Kupiga vita uongozi mbaya; pia mwandishi anapendekeza kuwa lazima tupige vita uongozi mbaya ili tukujenga jamii mpya. Mwandishi anamtumia mhusika Mwenyekiti kama kiongozi mbaya kwani anasikiliza upande mmoja wa mashitaka na kumlazimisha Bi. Nane kutoa maelezo kwa njia ya mdomo. Jambo linalopelekea Bi. Nane kukataa, kama inavyothibitishwa;

"Bi. Nane: Samahani mwenyekiti haki ni yangu ya kutoa maelezo kwa njia yoyote...."

Viongozi wa namna hii pia wapo katika jamii zetu kwani huongoza vibaya kwa kufuata matakwa yao. Hivyo mwandishi anasisitiza umuhimu wa kupiga vita uongozi mbaya uhenduwao na viongozi wetu.

Umuhimu wa elimu; jamii yoyote ili iweze kujengwa na kuwa mpya lazima elimu ithaminiwe mkazo. Mwandishi anaonyesha jinsi jamii

7 ya Patata uwepo wa elimu kwa baadhi ya watu. Hii inathibitishwa kwa kupitia mhusika Bi. Nane;
"... (Mkarara unaendelea): Anaingia Bi. Nane akiwa amevaa nguo za kisasa na vitabu vipataryo .......".
Pia wanawake wa Patata wanatilia mkazo katika somo la ushonaji ili tu kuleta maendeleo.
"... pia somo la ushonaji litatiliwa mkazo mashuleni ....".
Hivyo ili kujenga jamii yoyote ile hata katika jamii zetu hatuna budi kutilia mkazo suala zima la elimu. Hata kwenye jamii yetu uwepo wa elimu husaidia katika kujenga jamii mpya.
Kupiga vita umasikini; umasikini ni kikwazo katika kujenga jamii mpya. Umasikini mwandishi anaonyesha kwa kutumia wahusika Bi. Tano na Bi. Sudi. Sudi anakosa nguo za kuvaa kutokana na umasikini na kujikuta na nguo za kauka nikuvae. Pia Bi. Tano ~~bar~~ analalamika kuwa watoto wake wanalala na kukosa chakula;
"Bi. Tano: Taabu! Taabu! Taabu!
Wanangu wanalala njaa; hawana nguo --- pesa zote mwanaume hupeleka kwa wanawake ..."
Umasikini huletwa pia na sisi wenyewe hivyo hatuna budi kupiga vita umasikini na kufanya kazi kwa bidii ili tu kuweza kujenga jamii mpya isiyo na umasikini.
Kupiga vita dhuluma; dhuluma ni kitendo cha mtu kuchukua mali au kitu cha mtu pasipo ruhusa yake. Mwandishi

7 anaonyesha kuwa dhuluma ni chanzo cha kutoku-
wepo kwa jamii mpya. Bi. Saba anadhulumiwa
mali zake baada ya kifo cha mumewe. Hii ina-
onyeshwa anapolalamika;

"Bi. Saba: Haa! Shemeji mmerudi kuchuku-
a hata kitanda; hata sufuria; nitalala
wapi na kupikia wapi mimi - - . . ."

Hivyo msanii anapendekeza kupiga vita dhulu-
ma ili tuweze kujenga jamii mpya kwani
dhuluma ukwamisha maendeleo. Pia kuende-
lea na kitabu cha "Kivuli Kinaishi" mwandishi
anapendekeza mbinu zifuatazo;

kupiga vita matabaka, matabaka ni
utengano wa makundi mawili kiuchumi, kisiasa
au kiutamaduni. katika jamii ya Giningi kuna
tabaka tawala la Bi. Kirembwe, Wazee, Bawabu
na Mtangazaji wanaoonea tabaka la chini la
wali, wafanyakazi (tabibu na mkulima) Tabaka
tawaliwa linaonewa kwa kupewa adhabu
kali za kuondolewa viungo vya mwili. Hii
inadhihirishwa pale Bi. Kirembwe anapomhukumu
Mwalimu kwa kushindwa kufaulisha wanafu-
nzi;

"Bi. Kirembwe: Unalaaniwa na hamasa
sheria na kanuni za Giningi kuka-
twa ulimi unaokuringia - - - - -"

Tabaka tawaliwa linapata adhabu kali kwani
serikali haitoi vifaa vya kutosha kama vitabu;
matrekta na mbegu. Hivyo msanii anapendeke-
za kupiga matabaka ili kujenga jamii mpya
isiyokuwa na matabaka na itakayokuwa nzuri
kwa watu wote.

7. Kupiga vita uongozi mbaya; pia ili kuje-nga jamii mpya hakuna budi kupiga vita uongozi mbaya wa viongozi. Viongozi wa Giningi kama Bi. Kirembwe anajipa madaraka na kufanywa kuogopwa na watu. Kama inavyo-onyeshwa;

"Mtangazaji: Mfalme wa ufalme, mchawi wa wachawi mjua yote ya ndani na nje ya juu na ardhini - - -"

Hivyo ili kujenga jamii mpya msanii anapen-dekeza kuwa tupige vita uongozi mbaya.


Kupiga vita imani za kishirikina; pia mwandishi anapendekeza kuwa hakuna budi kupiga vita imani za kishirikina na potofu zilizopo katika jamii zetu. Bi. Kirembwe anao-nekana kama mtu mwenye nguvu kali.

"- - - mchawi wa wachawi mjua yote ya ndani na nje - - -"

Hivyo ili kuweza ku kuleta jamii mpya ni lazima tupige vita imani za kishirikina zilizo-po katika jamii zetu kwani hukwamisha maendeleo.

Umuhimu wa kujitoa muhanga; pia ili kuweza kujenga jamii mpya lazima wawepo watu wa kujitoa muhanga kama Mtolewa aliyejitolea ili ku kupiga vita uongozi mbaya wa Giningi. Yeye anajia-mini na kutoogopa chochote. Kama inavyo thibitishwa;

"- - - - najiamini kama mchawi yoyote yule anavyojiami ni - - - -"


7. Hivyo ili kuweza kujenga jamii mpya ni lazima wawepo watolewa wengi katika jamii zetu hususani jamii zilizojaa uongozi mbaya.
Umuhimu wa kufanya mapinduzi; pia ili kuweza kujenga jamii mpya ni lazima kufanya mapinduzi na kupindua uongozi mbaya. Hapa lazima kuwepo na elimu ili ku kusaidia watu katika kufanya mapinduzi. Elimu au unga wa ruhiba uliotolewa na Mtolewa kwa watu ulisaidia katika kufanya mapinduzi kwani waliweza kujua mabaya yote ya serikali. Hii inaonyeshwa na msanii;
"...Naona mmehiwa mzugo
Wali: Nyeusi ni nyeusi na nyeupe ni
nyeupe haiwezi kuwa manjano..."
Hivyo ili kujenga jamii mpya ni lazima kufanya mapinduzi.
Mwisho; waandishi wa tamthiliya hizi wamependekeza mbinu hizi kwani husaidia na huweza kusaidia katika kujenga jamii mpya zilizokuwa na rushwa, unyonyaji, ukoloni mamboleo na hali zote za uonevu.

Kielelezo 7.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kufafanua vizuri mbinu tano zilizopendekezwa na waandishi kama nyenzo za ujenzi wa jamii mpya.

Aidha, asilimia 11.5 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata alama za wastani ambazo ni kuanzia alama 7 hadi 11.5 kwa sababu waliweza kutaja matatizo yaliopo katika jamii bila ya kufafanua au kuonesha mbinu gani walizotumia waandishi ili kuweza kujenga jamii mpya katika kuleta maendeleo ya kweli.

Hata hivyo, wapo watahiniwa wachache sana (1.5%) waliopata alama 0 hadi 6.5. Miongoni mwao, asilimia 0.2 walishindwa kuhusisha mbinu mbalimbali zilizotumiwa na waandishi hivyo kupata alama 0. Kwa mfano, katika tamthiliya ya *Morani* mtahiniwa mmoja aliorodhesha; ‘‘*mbinu ya kutumia barua*’’, ‘‘*mbinu ya kutumia risasi*”, ‘‘*mbinu ya kutumia hadithi”*na *mbinu ya kutumia majibizano.*’’ Kwa upande wa tamthiliya ya

*Kivuli Kinaishi* mtahiniwa aliandika; ‘‘*mbinu ya kutumia uchawi*’’, ‘‘*mbinu ya kutumia sauti*’’, na ‘‘*mbinu ya kutumia nyimbo*’’ hoja ambazo hazikuwa mbinu sahihi katika kujenga jamii mpya. Kielelezo 7.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu tofauti na matakwa ya swali.

**Kielelezo 7.2**

7. Mbinu ya vyombo vya habari, kuonesha mchango wao katika ujenzi wa jamii mpya mfano pale walipotangaza kuwa kuna wahujumu uchumi 7000 wameshakamatwa tayari. Mbinu hii inaumuhimu kwa vile mwandishi anaeleza kuwa ili jamii yoyote ijengwe lazima kuwepo na vyombo vya habari.

Pia, Mbinu ya kutumia barua.

Vilevile, Mbinu ya kutumia risasi.

Mbinu ya kutumia hadithi

Mbinu ya kutumia Majibizano.

7. kwa upande wa tamthiliya ya kweli
kinaishi kama ifuatavyo.

Mbinu ya kutumia uchawi

Mbinu ya kutumia sauti

Mbinu ya kutumia hadithi, ambayo ni fasihi simulizi ndani ya fasihi andishi, pale Bi kizee alipowakusanya watoto; Na kuwahadithia juu ya mazimwi ya Giningi.

Pia, Mbinu ya kutumia nyimbo.

Kielelezo 7.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kutaja na kufafanua mbinu zilizotumiwa na waandishi wa tamthiliya kama nyenzo ya ujenzi wa jamii mpya katika kuleta maendeleo ya kweli.

### 3.5.2 Swali la 8: Uhakiki wa Tamthiliya

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Andishi*, lilihusu vitabu teule vya tamthiliya na lililenga kupima majazi ya utambuzi ngazi ya tathmini. Swali lilikuwa na jumla ya alama 20 na lilimtaka mtahiniwa afafanue kuhusu machungu yanayodhihirika katika tamthiliya mbili kutokana na ujumbe mzito unaobebwa kwa jamii.

Swali lilijibiwa na watahiniwa wachache (25.4%) kati ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Hata hivyo, asilimia 74.1 ya watahiniwa hao walilijibu vizuri na kupata alama 12 hadi 20. Baadhi ya watahiniwa hao waliopata alama za juu waliweza kufafanua machungu hayo kama, dhuluma iliyokuwa inafanywa na viongozi kwa wananchi, mila potofu zilivyokuwa zinamkandamiza mwanamke na wananchi kukosa haki yao kutokana na kushamiri kwa rushwa. Aidha, watahiniwa wengine waliofanya vizuri waliweza kuandika machungu hayo na kuyathibitisha kwa hoja zinazodhihirika kutoka katika vitabu teule vya tamthiliya. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kufafanua machungu hayo kama vile ; *Uhujumu uchumi*, *usaliti*, *rushwa*, *uongozi mbaya*, *kukosekana kwa haki* na *matabaka* kama mambo yanayoileteа jamii masikitiko makubwa na kuikosesha maendeleo ya kweli. Kielelezo 8.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kufafanua machungu yanayodhihirika katika tamthiliya mbili teule.

**Kielelezo 8.1**

8. Machungu: Ni mambo ambayo yanahuzunisha au kuleta masikitiko. Machungu humfanya mtu alie au kupata hasira. Ni kweli tamthilia nyingi zina machungu ambayo yanatokana na ujumbe kwa kutumia tamthiliya za KIVULI KINAISHI iliyotungwa na Said Mohamed na tamthiliya ya MORANI iliyotungwa na Emmanuel Mbogo nathibitisha machungu hayo nikianza na tamthiliya ya MORANI.

Uhujumu uchumi; Mwandishi kwa kutumia mhusika wake Nungunungu ameweza kuonesha jinsi alivyokuwa anahujumu uchumi ~~kwa~~ na kujenga hoteli nje na kuwa na akaunti Uswizi. Suala hili linaleta uchungu kwa ~~watu~~ wanajamii kwa sababu wanashindwa ~~ku~~endelea kutokana na viongozi kuwa wahujumu.

Usaliti; Vilevile kwa kutumia wahusika Mlemeta na Yusufu mwandishi anaonesha jinsi watu hao wanavyoshirikiana na Nungunungu na kuwaita kampuni za kuwakamata wahujumu uchumi. Suala hili pia linaleta uchungu kwa sababu uhujumu unaendelea na wananchi wanazidi kuteseka.

Rushwa: Vilevile mwandishi ameweza kuonesha suala la rushwa ambapo mwandishi anaelezea ~~Nungu nu~~ Mlemeta na Yusufu wamenunuliwa na Nungunungu. Rushwa pia inapatikana katika tabaka la juu yaani kina Nungunungu ambao

wanachukua rushwa ili kujiendeleza wenyewe hivyo suala hili linaleta uchungu. kwa sababu linanyima maendeleo katika jamii.


8. Watu wazima kutembea na watoto wadogo: Mwandishi kupitia Mhusika wake Nungunungu na Aisha ameonesha jinsi ambavyo nungunungu alivyo kuwa anafanya mapenzi na Aisha na mwishowe Aisha anafukuzwa shule. Pia suala hili linaleta uchungu kwa sababu watoto ambao ni tegemeo la Taifa wanaacha shule wakiwa bado wadogo.

Vilevile katika kitabu cha KIVULI KINAISHI mwandishi ameonesha Machungu mbalimbali yanayopatikana katika jamii. kutokana na ujumbe mzito unaobebwa na jamii

Rushwa: Mwandishi ameweza kujadili suala hili ~~kupitia~~ kupitia kwa ~~B~~ Mhusika Bawabu II ambapo anaonekana kuchukua rushwa ya shilingi 5000 kutoka kwa Mtolewa. Rushwa ni moja kati ya machungu katika jamii kwa sababu inapelekea kukosekana kwa haki.

Utawala wa Kimabavu au Utawala wa kidikteta, Hili linaonekana kupitia kwa Mhusika Bi Kirembwe ambaye yeye alitawala Giningi kwa Mabavu akiwaua watu na akiwaloga wari unga wa ndere. Suala la utawala wa Mabavu linaleta uchungu kwa ~~jamaa~~ jamii kwa sababu linasababisha ukosekanaji wa haki.

Kukosekana kwa haki, Pia suala la kukosekana kwa haki limetokea katika familia ya kivuli kinaishi kwa sababu tunaona ~~ji~~ jinsi watu wananyimwa uhuru wa kuongea na ~~kujieleza~~ kujielezea kama alivyokuwa kwa wari na



walimu, Hivyo suala la kukosekana kwa haki linaleta uchungu kwa sababu linasababisha watu kushindwa kufikia malengo yao.

8 Matabaka: Said Mohamed amejadili suala la matabaka kuamba kuna tabaka la juu wenye nacho likiwakilishwa na Bi Kirembwe, Mtangazaji, wazee na Bawabu I na II na pia tabaka la chini ambalo linawakilishwa na Mtolewa, wari, Mwalimu, Daktari na wengi. hivyo suala hili linaleto uchungu sana katika jamii.

Mwisho: Mwandishi ametoa masuluhisho ili kuweza kuondokana na uchungu huo Masuluhisho hayo ni kama vile kujitoa muhanga na kufanya Mapinduzi kwa hivyo hayo ni masuluhisho yaliyopendekezwa na Mwandishi

Kielelezo 8.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa ambaye aliweza kutoa hoja mbalimbali zinazoleta machungu na masikitiko makubwa kwa jamii.

Aidha, asilimia 22.7 ya watahiniwa waliofanya swali hili walishindwa kufafanua baadhi ya hoja ingawa waliweza kuzitaja. Hata hivyo, maelezo ya watahiniwa hao hayakuwa na ufafanuzi toshelevu hivyo kupata alama za wastani ambazo ni kuanzia alama 7 hadi 11.5.

Licha ya swali hili kujibiwa na watahiniwa wachache na kufanywa vizuri na asilimia kubwa ya watahiniwa (74.1%), asilimia 3.2 walishindwa kulijibu kwa usahihi na hivyo kupata chini ya alama 7 ambazo zilikuwa alama za wastani. Miongoni mwa watahiniwa hao, asilimia 0.2 walipata alama 0 kutokana na kutokuwa na maarifa ya kutosha na kutoelewa mahitaji ya swali kuhusu machungu yanayodhihirika ambayo yanabeba

ujumbe mzito wenye masikitiko makubwa kwa jamii. Aidha, watahiniwa wengine walieleza hoja ambazo hazikuwa majibu sahihi ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza kuhusu dhamira ambazo hazikuwa zinalandana na matakwa ya swali kama Kielelezo 8.2 kinavyoonesha.

**Kielelezo 8.2**

8 Ujumbe ni kile kitu ambacho
mwandishi hukiandika kwa ajili ya
jamii yake kujifunza juu ya mambo
fulani. Katika Tamthiliya mbili ambazo
ni Morani na Kwenye Ukingo wa Thim
mwandishi ameweza kuibua ujumbe
wa aina mbalimbali kwa ajili ya
kujifunza zaidi jamii yake. Ujumbe
ambao mwandishi ameutumia ni Ujumbe
ambao una machungu na mzito unaobe
bwa kijamii na kuibua hisia za
watu wengi. ~~Ufuatar~~ Zifuatazo ni
Jumbe mbalimbali ambazo mwandishi
au waandishi wametumia katika kuibua
machungu na hisia za watu, Katika
tamthiliya ya Morani Mwandishi Emma
nueli Mbogo ametoa ujumbe kama
ifuatavyo;
Umuhimu wa elimu, katika
tamthiliya ya Morani mwandishi
ameweza kuasa jamii yake juu
ya umuhimu wa elimu kwa kumt
umia mhusika Aisha ambaye haku-
ona umuhimu wa elimu pale alipoku
a akitumia mda mwingi kwenda
kwenye klabu usiku na Nangunungu
badala ya kusoma na mwishowe
kufukuzwa kazi.
Umoja na mshikamano, Emman-
uel Mbogo ametuasa kama wana
jamii wenzake katika suala la
kuwa na umoja na mshikamano

8 ili kuweza kufanikisha na kuleta
maendeleo katika jamii zetu. Mwa-
ndishi amewatumia wahusika kama
Jalia na wenzake walipokuwa wa
wanahangaikia haki za wananchi
zinazochukuliwa na wahujumu uchumi
Rushwa haifai, katika tamthiliya
ya Morani mwandishi ameonyesha
jinsi rushwa inavyoweza kuharibu
maendeleo ya jamii. Amemtumia
mhusika Kungu pale alipokuwa
anawaambia vijana wake kuwa
ataongea na advokate ili akifika
mahakamani ashinde kesi.
Kuwa na mapenzi mema na
nchi yetu, Mwandishi wa tamthiliya
hii pia ametoa ujumbe wa kuwaasa
wanajamii kuipenda nchi yetu kwa
dhati kwani ndipo tulipozaliwa. Amemtu-
mia mhusika Jalia pale alipokuwa
katika harakati za kutokomeza
uhujumu uchumi. Katika tamthiliya
ya Kwenye Ukingo wa Thim mwa-
ndishi ametoa ujumbe ufuatao;
Umuhimu wa ~~kisa~~ wosia, katika
familia zetu wosia ni muhimu
sana hasa pale mhusika wa
mali anapofariki wosia ule utawa
saidia ndugu na jamaa zake
katika uangalizi wa mali. Mwandishi
amemtumia mhusika Herbert mume
wa Martha ambaye hakuandika

Kielelezo 8.2 kinaonesha sampuli ya sehemu ya jibu la mtahiniwa aliyefafanua dhamira mbalimbali badala ya kueleza machungu yaliyodhihirika katika tamthiliya mbili teule.


## 3.6 SEHEMU E: USANIFU WA MAANDISHI.

### 3.6.1 Swali la 9: Usanifu wa Maandishi

Swali lilitoka katika mada ya *Usanifu wa Maandishi* na lilimtaka mtahiniwa asome shairi kisha ajibu maswali yaliyofuata; maswali hayo yaligawanyika katika vipengele (a) hadi (d) na vilikuwa na jumla ya alama 20.

Kipengele (a) kilimtaka mtahiniwa kupendekeza kichwa cha shairi kisichozidi maneno mawili. Kipengele (b) kilimtaka mtahiniwa kueleza dhamira ya mtunzi wa shairi kwa kutoa hoja nne. Kipengele (c) kilimtaka mtahiniwa kueleza maana za maneno kama yalivyotumika katika shairi. Maneno hayo yalikuwa (i) Kedi, (ii) Weledi, (iii) Tufani na (iv) Ubazazi. Kipengele (d) kilimtaka mtahiniwa aeleze kuhusu usemi alioutumia mshairi usemao, ‘‘Achumacho ni posho’’.

Swali lilijibiwa na watahiniwa wachache (37.5%) kati ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili na kufaulu kwao kiasilimia kumewasilishwa vizuri katika Chati Na. 9 kwa kuonesha kufaulu kwa kiwango hafifu, kufaulu kwa kiwango cha wastani na kufaulu kwa kiwango kizuri.




**Chati Na. 9**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Asilimia 84.1 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 7 hadi 19.5. Aidha, asilimia 30 ya watahiniwa waliolijibu walipata alama 12 hadi 19.5. Idadi kubwa ya watahiniwa waliofanya vizuri waliweza kujibu sehemu kubwa ya swali kwa usahihi kutokana na uelewa mzuri wa matini waliyoisoma katika shairi walilopewa. Aidha, watahiniwa wachache waliolijibu waliacha baadhi ya vipengele kutokana na kukosa uelewa wa matini waliyopewa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliyejibu vizuri alishindwa kujibu kipengele 9 (b) (i) kwa kuandika, *kutetea maslahi ya wanyonge* badala ya kuandika *umuhimu wa kufanya kazi ili kujikwamua kimaisha*. Katika kipengele (b) (iii) mtahiniwa aliandika, *kupinga rusha* badala ya *rushwa* na kupata alama pungufu kutokana na tatizo la kitahajia. Kielelezo 9.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri na kupata alama za juu.

**Kielelezo 9.1**

9. a) WAVUJA JASHO

b) Dhamira ya mtunzi ni:

i) Kutetea maslahi ya wanyonge – mtunzi ameonyesha dhamira hii katika ubeti wa ~~sita~~ tano anaposema

"Lazima waungane
Wanyonge:
"Na wafanyakazi,
Hulia mia ujuzi,
Kuchapa sana kazi,
Kazi wanaienzi,
Kwa huba na mapenzi,
Bila ya ubezazi,
Lakini malofa"


ii) Kuhimiza umoja – Hii ameionyesha katika ubeti wa sita, anasema

"Lazima waungane
Wanyonge washikane.

iii) Kupinga rushwa – dhamira hii imeonyeshwa katika ubeti wa mwisho

iv) Uongozi mbaya – ~~mw~~ mtunzi ameeleza dhamira hii katika ubeti wa mwisho, ambapo ameonyesha jinsi viongozi wanavyo watesa raia wao, kwa kula rushwa mtunzi anasema,

"Maafisa balaa
Rushwa imezagaa
Uozo ulioja
Hakuna manufaa


9. c) i) Kedi - Neno hili lina maana ya kiburi

ii) Weledi - Ujuzi wa kutenda jambo fulani

iii) Tufani - Ni upepo mkali

iv) Ubazazi - ~~H~~ Lina maana ya udanganyifu.

d) Msanii anaposema "Achumacho ni posho" anamaanisha kuwa watu wanyonge kile wanacho kipata kupitia shughuli zao kama vile kilimo na uvuvi ndio malipo ~~k~~ yao, malipo ambayo huwafanya wajikimu kwa maisha yao. Ambapo wanacho kichuma ni kidogo sana.

Kielelezo 9.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kujibu kwa usahihi vipengele vingi vitokanavyo na shairi alilopewa.

Aidha, asilimia 54.1 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 7 hadi 11.5 ambazo ni alama za wastani kwa sababu walishindwa kujibu baadhi ya vipengele vya swali hili kwa usahihi. Miongoni mwa watahiniwa hao, katika kipengele cha 9 (c) walishindwa kutoa maana sahihi ya maneno yote kama yalivyotumika katika shairi. Pia baadhi ya watahiniwa walishindwa kunukuu neno *Bazazi* na kuandika *Babazi* jambo linaloashiria kuwa huenda waliathiriwa na lugha mama. Hata hivyo, watahiniwa wengine hawakuwa na uelewa mpana wa baadhi ya istilahi kama zilizotumika katika shairi husika. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliruka kipengele (i) hadi (ii) kama Kielelezo 9.2 kinavyoonesha.

**Kielelezo 9.2**

9.b/. ii/. Suala la rushwa.

—Msanii ameonesha jinsi rushwa ilivyo adui wa haki na inavyopotosha maadili ya uongozi. Kwa mfano katika ushairi ufuatao;

"Rushwa mezagaa
Uozo ulivojaa".

iii/. Umoja na mshikamano

—Ili wananchi waweze kupata maendeleo ni lazima waungane katika kuhakikisha maovu bila hofu.

Mfano;

"Lazima waungane
Wanyonge washikane
Na washirikiane
Dhuluma waikane"


iv/. Bidii katika kazi

—Ili watu waweze kufanikiwa ni lazima wajitume kwa ajili ya kuweza kujipatia kipato cha kuwawezesha kupata mahitaji muhimu ya maishani.

Mfano katika ushairi ubeti wa kwanza;

"Kila mvuja jasho
Mashaye ya kesho
Si ya utajisho
Achumacho ni posho"

C/. i/. Kedi – ni hali ya kutokuwa katika shughuli katika kwa watu yeyote.



9. c/. ii/. Weledi - ni ile hali ya kuwa na busara na matumaini ya kufanyika kwa jambo fulani hapo baadae

iii/. Tufani - ni hali ya tafrani inayosababishwa na upepo mkali unaoambatana na mvua ya radi.


iv/. Ubabazi - ni hali ya kutokuwa na mgomo kabla kujitia kufanya kazi.

d/. Mshairi anamaanisha kuwa kile anachokipata mtu kutokana na kujituma katika kazi ndio mshahara wake kwa kuwa riziki aitafutayo mtu huwa ni kutokana na kufanya kazi

Kielelezo 9.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye alipata alama za wastani kutokana na kushindwa kujibu kwa usahihi vipengele 9 (a), 9 (b) (i), 9 (c) (i) na (b) (iv) jambo lililosababisha kutokupata alama zote.

Asilimia 15.9 ya watahiniwa waliojibu swali hili walishindwa kulielewa shairi na hivyo kutokujibu maswali yahusuyo shairi hilo ipasavyo. Pia baadhi ya watahiniwa hao, waliruka kipengele (i) na (ii). Aidha, watahiniwa wengine katika kipengele cha (iii) na cha (iv) walishindwa kutoa maana sahihi ya maneno kama yalivyotumika katika shairi na hata kushindwa kuyanakili maneno hayo kwa usahihi hivyo kupata alama 0 hadi 6.5 ambazo ni chini ya wastani. Kati ya watahiniwa hao, asilimia 0.3 walipata alama 0 kwa kushindwa kuelewa maudhui ya shairi ambayo yalilenga katika umuhimu wa kufanya kazi kwa umoja na mshikamano ili kupata maendeleo ya kweli na kupinga uongozi uliojaa rushwa na dhuluma. Kielelezo 9.3 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa ambaye hakuelewa vema maudhui ya shairi.

**Kielelezo 9.3**


7 (a) Bidii kutofanikiwa

(b) i/ Kufanya kazi kwa kuwaza jamii kutojituma, kazi kuonekana

ii/ Jamii kukata tamaa katika kufanya kazi

iii/

iv/

c/ i/ Kutofanikiwa

ii/ kwa juhudi


iii/ Malimbi kazini

f/. Kpatacho

Kielelezo 9.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa ambaye hakuelewa maudhui ya shairi hivyo kushindwa kutoa majibu sahihi.

### 3.6.2 Swali la 10: Usanifu wa Maandishi

Swali lilitoka katika mada ya *Usanifu wa Maandishi* na lilimtaka mtahiniwa kusoma kifungu cha habari na kisha kujadili mbinu za kifani zilizotumika kufikisha ujumbe. Swali lilikuwa na jumla ya alama 20 na lililenga kupima majazi ya utambuzi katika ngazi ya uchambuzi. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili na kufaulu kwao kiasilimia kumefafanuliwa vizuri katika Chati Na.10 kwa kuonesha kufaulu kwa kiwango hafifu, kufaulu kwa kiwango cha wastani na kufaulu kwa kiwango kizuri.




**Chati Na. 10**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Asilimia 79.6 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 7 hadi 19. Miongoni mwa watahiniwa hao asilimia 21.8 walilijibu vizuri na kupata alama 12 hadi 19. Watahiniwa hao waliweza kueleza mbinu za kifani zilizotumika katika habari waliyopewa katika viwango tofauti. Baadhi ya watahiniwa hao waliopata alama za juu walieleza vipengele vya fani kama vile ; mtindo, muundo na matumizi ya lugha. Aidha, watahiniwa wengine walijikita kueleza vipengele vilivyohusu wahusika, mandhari, tamathali za semi, misemo, methali na nahau. Kielelezo 10.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili kwa kueleza mbinu mbali mbali za kifani zilizotumika katika habari waliyopewa kama vile : *muundo uliotumika kuwa wa moja kwa moja*, *mtindo wa masimulizi*, *matumizi ya nafsi ya kwanza na ya tatu wingi katika sentensi*, *wahusika (Simba, Ndege, Nyangichuro), mandhari (nchi, Afrika), matumizi ya lugha, tamathali za semi* kama vile ; *tashbiha, sitiari na tashhisi* pamoja na mbinu nyingine za kisanaa.

**Kielelezo 10.1**


10 Kufafanua mbinu za kifani zilizotumika kufikisha ujumbe.

(a) Muundo
- Mwandishi ametumia muundo wa moja kwa moja. Ameonesha mzee Karugamba alipojisemea maneno ya kulalamika na kuamua kuchukua hatua. Pia ameonesha Nyagichuro alivyompinga na malalamiko ya wengine juu ya uongozi wa Senangu Isakuro na ba. mwisho mwandishi anaonesha kuwa mawazo yao yalifungua macho ya wengi

b) Mtindo
Mwandishi ametumia mtindo wa masimulizi pia ametumia nukuu mbalimbali.
Mwandishi ametumia pia nafsi
mfano
Nafsi ya tatu wingi - wanawake wanavaa
Nafsi ya kwanza Wingi - Tumelaaniwa

c) Wahusika.
- Nyagichuro
- Senangu Isakuro
- Mzee Karugamba
- Wanawake na Wasichana
- Gekorara
- Simba
- Ndege

d) Mandhari
- Nchini, Afrika,


10

(e) Matumizi ya Lugha.

(i) Misemo na Nahau

- Inayovuja jasho - Usingizi wa mang'amng'am
- Akina baba kabwela - Taabani
- Kila jambo lina mwisho wake.
- Hatuna budi kujiuliza maswali

(ii) Methali

- leo ni leo asemaye kesho ni mwongo
- Kikulacho ki nguoni mwako.
- Penye miti hakuna wajenzi

(iii) Tamathali za semi

(i) Tashibiha

- Nyekundu mithili ya moto
- Wajanja kama sungura
- Moto mfano wa radi

• Sitiari

- Sisi si mbwa mwitu. - Waliti ni chanzo cha maovu
- Sisi ni wajanja

• Tashihisi

- Giza totoro limevamia nchi
- Machungu yanatuchemka
- Ndege wa angani waishio katika anga letu wazi-di kusononeka.

Kielelezo 10.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kujibu vizuri kwa kueleza mbinu za kifani zilizotumika katika habari aliyopewa.

Hata hivyo, asilimia 57.8 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 7 hadi 11.5 ambazo ni alama za wastani. Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha ya kutambua mbinu mbalimbali za kifani zilizotumika katika kifungu cha habari. Baadhi yao waliweza kuzitambua mbinu chache za kifani kama vile muundo, mtindo na matumizi ya lugha lakini wakashindwa kufanya rejea katika habari waliyopewa. Watahiniwa wengine waliweza kuzitambua lakini walishindwa kuzifafanua ipasavyo kwa kutumia mifano dhahiri kutoka katika kifungu cha habari. Kielelezo 10.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye aliweza kutambua baadhi ya mbinu za kifani zilizotumika ingawa hakuweza kutoa ufafanuzi uliokuwa toshelevu, hivyo kupata alama za wastani.

**Kielelezo 10.2**

Fani ni ufundi anaoutumia mwand-
10. ishi wa kazi ya fasihi katika kujenga
kazi yake. Pia fani imegawanyika au hu
angaliwa katika vipengele vifuatavyo
Muundo, Mtindo, Wahusika, Mandhari-
Matumizi ya lugha. Kupitia habari hii
tunaanza na kuchambua vitu vifuatavyo
Muundo, Ni mgawanyiko wa visa
na matukio katika fasihi andishi na
pia muundo wa habari hii ni mojakwa
moja, kwa sababu ulianza na jinsi wanawa-
ke wana vyoaribika na ~~utatao~~ utamaduni
wa nchi za ughaibuni na jinsi ganiwa
nanchi wanavyotawaliwa, pia kuna aya tano.
Mtindo, ni ufundi anaoutumia -
mwandishi kujenga kazi yake. Mtindo ni
wa Monolojia ambao ni maelezo juu
ya jamii ya sasa jinsi ilivyo haribika
na tamaduni za nje.
Wahusika, ni watu wanaojengwa kiya-
kinifu na mwandishi, pia mwandishi ame
tumia majina ya watu kama. Mzee Karu
gamba, Nyagichuro, Sanegu Isakuro ambao
wanaelezea uongozi na jinsi jamii ilivyo
badilika na utandawazi
Mandhari, ni sehemu au mahari amb
apo kazi ya fasihi hufanyika, inaweza ku
wa ya kubuni au halisi, Mandhari ya
habari hii ni ya kubuni ambapo ametu
mia nchi kuonyesha matatizo.
Matumizi ya lugha, msanii hutumia
methali, misemo nahau, tamathali za -

10 semi katika kujenga kazi yake ame
tumia baadhi ya methali kama vile.
' 'Methali, ni semi zenye pande
mbili zenye kuleta busara na hekima
Pia kwenye kifungu cha habari kuna
methali zifuatazo.
"Kikulacho kinguoni mwako"
ikimaanisha adui hatokei mbali.
"leo ni leo asemaye kesho mwa
ngo" alipokuwa akieleza juu ya nchi.
Penye miti mingi hakuna ....
Pia kuna tamathali za semi zime
tumika kama vile takriri
Takriri kujirudia rudia kwa
maneno mfano.
Usaliti!, usaliti! usaliti
Mjalizo kufuatana kwa maneno
yasiyokuwa na maana mfano.
Je, tuko wapi? Je tutafika
Je tunaelekea wapi je tunatoka wapi
Kupuuzwa! kudharauliwa
kudhihakiwa! inatosha.
Ujumbe, katika habari hii mwa
ndishi ameonesha yapaswa tuwe na tam
aduni za kwetu na sio kufuata za nje
pia anaonesha umuhimu wa kuwa na
tamaduni za kiafrika na kusababisha
maendeleo.

Kielelezo 10.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye aliweza kuzitambua baadhi ya mbinu zilizotumika japo hakuweza kuzifafanua ipasavyo kwa kutumia mifano kutoka katika kifungu cha habari, hivyo kupata alama za wastani.

Aidha, asilimia 20.4 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 0 hadi 6.5 ambazo ni alama chini ya wastani. Watahiniwa hao walishindwa kueleza mbinu mbalimbali za kifani zilizotumika katika kifungu cha habari kama vile; mtindo na muundo wa kifungu cha habari, wahusika, mandhari, matumizi ya nafsi na matumizi ya lugha. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika kipengele kuhusu misemo ambacho ni sehemu tu ya matumizi ya lugha kama Kielelezo 10.3 kinavyoonesha.

**Kielelezo 10.3**

10 i, Tashibiha - Kulinganisha vitu viwili au mambo mawili kwa kutumia maneno kama " mithili ya, kama na mengine mengi

mfano

" Nchi ambayo wanawake huvaa nywele za -. Nchi ambayo wasichana huwagiza nywele zao ili ziwe nyekundu mithili ya moto

ii, Takriri - Ni kurudia rudia maneno

mfano

" Usaliti ! usaliti ! usaliti ! Tena usaliti

iii, Tashihisi - Kuunganisha mambo mawili yasiyo na uwiano bila kutumia kuunganishi

Mfano

Nchi ambayo inanuka damu

iv, Mdokezo - Kutomalizika kwa sentensi

mfano

Nchi ambayo wanawake huvaa nguo.......

Nchi ambayo wanawake huvaa nywele za - ......! haya ndiyo maendeleo yetu ...

v, Misemo Methali

mfano

Penye miti mingi hakuna ...!

Kielelezo 10.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye hakuweza kueleza mbinu zote za kifani zilizotumika katika kifungu cha habari isipokuwa aliweza kutambua kipengele kimoja tu cha matumizi ya misemo.

## 4.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA KUFAULU CHA WATAHINIWA KWA MADA

Kiwango cha kufaulu katika mada zilizotahiniwa mwaka 2016 kilikuwa kizuri ambapo asilimia 96.94 ya watahiniwa walipata wastani wa alama 35 na zaidi. Kiwango hiki cha kufaulu kimekuwa na upungufu wa asilimia 0.02 ikilinganishwa na kiwango cha kufaulu cha mwaka 2015 ambapo kiwango cha wastani cha kufaulu kilikuwa 96.96.

Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika mada za mtihani wa 121/1 Kiswahili 1 kinaonesha kuwa watahiniwa walifanya vizuri katika mada zote hasa katika mada ya *Utumizi wa Lugha* ambapo ufaulu ulikuwa ni asilimia 98.1, *Ufahamu na Ufupisho* asilimia 95.7, *Maendeleo ya Kiswahili* asilimia 95.6, *Matumizi ya Sarufi* asilimia 68.7 na *Tafsiri na Ukalimani* asilimia 66.2. Aidha, kiwango cha kufaulu katika mada za *Matumizi ya Sarufi* na *Tafsiri na Ukalimani* kilikuwa kizuri ila kwa kiwango cha chini kidogo kikilinganishwa na mada nyingine.

Hata hivyo, katika mtihani wa 121/2 Kiswahili 2, watahiniwa wengi walifanya vizuri katika mada zote. Kufaulu kwa watahiniwa katika mada hizo kulikuwa kama ifuatavyo:- *Ushairi* asilimia 98.7, *Riwaya* asilimia 98.5, *Tamthiliya* asilimia 97.7, *Fasihi kwa Ujumla* asilimia 92.4 na *Usanifu wa Maandishi* asilimia 81.9.

Uchambuzi wa viwango vya kufaulu kwa mtihani huu unaonesha kuwa watahiniwa walifanya vizuri katika mada zote. Kufaulu kwa kiwango kizuri kwa mwaka 2016 kumetokana na watahiniwa wengi kuwa na ujuzi na weledi wa kutosha kuhusu mada mbalimbali zilizotahiniwa

## 5.0 HITIMISHO

Kwa ujumla mtihani wa somo la Kiswahili mwaka 2016 ulizingatia muhtasari wa somo la Kiswahili na ulizingatia majazi yote ya utambuzi kama vile maarifa, ufahamu, matumizi, uchambuzi, uundaji na tathmini. Kwa ujumla kiwango cha kufaulu kwa mwaka 2016 kilikuwa kizuri kwa kuwa wastani wa kiwango hicho katika mada zote kilikuwa ni asilimia **99.94**.

Uchambuzi uliofanyika unaonesha changamoto mbalimbali za watahiniwa wachache walioshindwa kufanya vizuri kama vile; uelewa mdogo wa matakwa ya swali, mtiririko usiokidhi vigezo vya uandishi, uelewa mdogo wa mada mbalimbali na uwezo mdogo katika kujibu maswali. Kadhalika, watahiniwa hao walishindwa kutoa mifano sahihi na ya kutosha katika kujenga hoja za kujibu swali na kutokufuata maelekezo ya swali.

Taarifa hii itasaidia kuinua kiwango cha kufaulu katika somo la Kiswahili kwani itatoa changamoto kwa walimu na wawezeshaji katika ufundishaji wa mada zilizoonekana kuwa na matatizo. Aidha, itatoa changamoto kwa wanafunzi na kuwahamasisha katika ujifunzaji wa mada zote za Kiswahili ili kuwapa uwezo wa kufahamu vizuri lugha ya Kiswahili na hatimaye kufanya vizuri katika somo la Kiswahili.

Mwisho, taarifa hii ya watahini kuhusu kufaulu kwa watahiniwa iwe changamoto katika kuwasaidia walimu na wanafunzi kuyaelewa makosa yanayosababisha watahiniwa wachache kutokujibu vizuri maswali na kisha kurekebisha kasoro hizo. Aidha, taarifa hii itakuwa ni tija kwa walimu katika ufundishaji, utungaji na usahihishaji wa mitihani, na hasa itasaidia kuinua kiwango zaidi cha kufaulu katika somo hili kwa kufanya Matokeo Makubwa sasa ya Kielimu kuwezekana kupitia lugha ya Kiswahili. Pia taarifa hii itatoa hamasa kwa wanafunzi na hasa ikizingatiwa kuwa Kiswahili ni lugha ya Taifa ambapo kila mtahiniwa anapaswa kujieleza vizuri bila kikwazo chochote huku akijiamini na kujivunia kuwa lugha hii ni sehemu ya utamaduni wa Mtanzania.

## 6.0 MAPENDEKEZO

Ili kuinua kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi inapendekezwa kuwa:

(a) Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa Elimu waandae warsha kuhusu mada za ; *Sarufi*, *Maendeleo ya Kiswahili*, *Tafsiri na Ukalimani*, *Historia ya Fasihi* na *Usanifu wa Maandishi* ili kuwapa fursa waalimu wa somo la Kiswahili kujifunza na kuongeza ujuzi katika ufundishaji wa somo hili.

(b) Wizara ya TAMISEMI kitengo kinachoshughulikia elimu kiandae semina elekezi kwa walimu wa Kiswahili ili kuongeza ujuzi zaidi kwenye baadhi ya mada kama mada za *Sarufi* na *Tafsiri na Ukalimani*.

(c) Wanafunzi wahamasishwe kujifunza zaidi mada ya *Sarufi*, *Tafsiri na Ukalimani* na mada za *Fasihi*. Aidha, kipengele cha fani katika uchambuzi wa vitabu na katika mada ya *Usanifu wa Maandishi* kipewe

kipaumbele zaidi hasa katika kusoma habari na kuweza kujua mbinu za kifani zilizotumika katika kufikisha ujumbe.

**Kiambatisho A**

# UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA KUFAULU KWA WATAHINIWA KWA MADA

## 121 KISWAHILI

| S/N | Mada | MTIHANI WA ACSEE - 2016 | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Idadi ya Maswali | Asilimia ya Watahiniwa Waliopata Wastani wa Alama 35 au Zaidi | Maoni |
| 1 | *Ushairi* | 2 | 98.7 | Vizuri |
| 2 | *Riwaya* | 2 | 98.5 | Vizuri |
| 3 | *Utumizi wa Lugha* | 1 | 98.1 | Vizuri |
| 4 | *Tamthiliya* | 2 | 97.7 | Vizuri |
| 5 | *Utungaji* | 1 | 96.1 | Vizuri |
| 6 | *Ufahamu na Ufupisho* | 2 | 95.7 | Vizuri |
| 7 | *Maendeleo ya Kiswahili* | 2 | 95.6 | Vizuri |
| 8 | *Fasihi kwa Ujumla* | 2 | 92.4 | Vizuri |
| 9 | *Usanifu wa Maandishi* | 2 | 81.9 | Vizuri |
| 10 | *Sarufi* | 3 | 68.7 | Vizuri |
| 11 | *Tafsiri na Ukalimani* | 1 | 66.2 | Vizuri |

Kiambatisho B

# UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA KUFAULU KWA WATAHINIWA KWA MADA

## 121 – KISWAHILI - 2016

